SUPA JACKPOT
TZS. 1,109,975,029
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Sakata** ununuzi Tanga Cement latikisa Bunge

UKURASA 3


Hili la vyeti vya udereva kwa kweli, halijakaa sawa
BUFE
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Uwanja wa Ndege Moshi, miaka 59 ukisuasua, lakini ni nyeti kiuchumi
UCHUMI
Dondoo Rais Samia zilivyowakuna wafanyakazi kwenye Mei Mosi yao

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Mei 5, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581301

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




# Jaji: Niliumizwa na Waziri Mkuu kuchana hukumu

• **Aanika** ukakasi 'vigogo' serikalini kuidharau mahakama... *Endelea ukurasa 2*




Bodaboda akiwa amepakia abiria na mifugo katika Barabara ya Morogoro, eneo la Mlandizi mkoani Pwani mwanzoni mwa juma hili, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria za usalama barabarani. **PICHA: SANULA ATHANAS**

## Wanafunzi wafariki wakimsaidia fundi ujenzi ukuta shule

UKURASA 3



MOTO JIMBO LA MBEYA

## Spika Tulia amwalika Sugu wachuane, aahidi kumfyeka

UKURASA 2

**MICHEZO** ROBERTINHO ATAKA STRAIKA, BEKI MPYA UK.24 **KATUNI** UK.6



Watuhumiwa wa kosa la kupatikana na bangi kilo 59, James Mayunga (wa pili kulia) na mwenzake, Scola Kashinde, wakiwa wameficha sura zao kukwepa kupigwa picha baada ya kutoka katika Chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana kusikiliza kesi inayowakabili. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Jaji: Niliumizwa Waziri Mkuu kuichana hukumu niliyoitoa

**Na Kulwa Mzee**

JAJI mstaafu John Mgeta amesema changamoto iliyomuumiza katika kutekeleza majukumu yake ni kitendo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, kudharau uamuzi wa mahakama kwa kuchana uamuzi aliotoa katika kesi ya mgogoro wa ardhi.

Jaji Mgeta alitoa kauli hiyo jana Mahakama Kuu Masijala Kuu Dar es Salaam katika hafla ya kitaaluma ya kuwaaga majaji wastaafu, Jaji Mgeta, Jaji Beatrice Mutungi na Jaji Sekela Moshi.

"Kuna changamoto katika mahakama ambayo bado mpaka sasa ipo - serikali kuingilia uamuzi wa mahakama na pia kama serikali ilishtakiwa ikashindwa utekelezaji wa amri ya mahakama unakuwa mgumu.

"Simaanishi kutoa maelekezo bali kushindwa kutekeleza uamuzi. Ni ngumu kuelezea sababu ni utashi tu wa mamlaka. Meno yaliyopo katika mahakama ni kuagiza tu maelekezo fulani yafanyike basi, hakuna mamlaka labda ya kuagiza kukamata au vipi!" alisema.

Jaji Mgeta alishauri mamlaka ya juu iwe inatoa maagizo kwamba maagizo ya mahakama yawe yanatekekezwa, akitolea mfano mkurugenzi mtendaji wa halmashauri akishindwa, mamlaka za juu zishinikize uamuzi utekelezwe.

"Kesi moja niliyoisikiliza nikiwa Arusha, nikatoa uamuzi mwanakijiji aliporwa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa shule. Akataka afidiwe, nikatoa uamuzi ukapelekwa kijijini kwa ajili ya utekelezaji lakini alikuwapo mkuu mmoja, akiwa likizo huko kijijini alichana ule uamuzi.

"Aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo jina simkumbuki, alikuwa anatokea Monduli. Aliniumiza sana kuona kwamba mahakama haikuthaminiwa. Shule ilienelea kujengwa lakini baadaye yule mwanakijiji alifidiwa baada ya mahakama kudharauliwa," alisema Jaji Mgeta.

Jaji huyo pia aliwataka majaji kudhibiti mienendo ya mashauri. Wasitoe mwanya wa uvivu na uzembe katika kutoa haki na wasiahirishe mashauri bila sababu za msingi.

Jaji huyo aliitumikia mahakama kwa miaka 32 katika nyadhifa mbalimbali ikiwamo uhakimu hadi alipoteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu Juni mwaka 2012.

"Katika miaka niliyofanya kazi nilihakikisha ninatekeleza majukumu yangu kwa uaminifu na kwa ukamilifu ili kutoa haki kwa jamii kwa wakati na kwa kiwango bora.

"Ninawasihi majaji, watekeleze wajibu kwa haki, uaminifu, kwa kufuata maadili na weledi kwa kuzingatia miiko na ushirikiano baina yao.

"Waimarishe ushirikiano na wadau wengine wa mahakama. Nimejifunza kuwa kazi za mahakama zinahitaji kutekelezwa kwa uhuru na uadilifu," alisema Jaji Mgeta.

Alisema uadilifu katika utendaji wa kazi za mahakama unadumisha sifa nzuri ya mahakama, utawala bora wa sheria utaonekana umeimarishwa na Tanzania kuonekana ni nchi ya kidemokrasia.

Jaji mstaafu Sekela aliyeitumikia mahakama kwa miaka 33, alisema anawakumbusha mawakili kuzingatia shajara ili kuepuka kuwa na mashauri mengi huku mengine yakiwa yanaahirishwa.

Alisema anawashukuru wadau wote wa mahakama wakiwamo Jeshi la Polisi na Magereza kwa kuwa kila mdau wa mahakama anayo nafasi yake katika kuhakikisha haki inatendeka.

"Ukiwa jaji kuna kazi nyingi. Kuna kuandika uamuzi na hukumu. Kazi ya ujaji inahitaji kujituma sana," alisema Jaji Sekela wakati akiaga na kuwashukuru majaji na watumishi wa mahakama kwa ushirikiano waliompa.

Jaji mstaafu Beatrice alitoa rai kwa majaji kujenga tabia ya kusoma na kufanya utafiti kabla ya kutoa uamuzi.

Jaji Mutungi aliyefanya kazi kwa miaka 33, alisisitiza mchakato wa Mahakama Mtandao upewe kipaumbele na kutoa mafunzo kwa watumishi, majaji na mahakimu.

" Wawapo watumishi wa kutosha, maslahi ya watumishi yaangaliwe ili kuepusha vishawishi. Sina shaka ninaondoka mahakama ninaiacha katika mikono salama," alisema.

Majaji wote wastaafu walizishukuru familia zao kwa kuwavumilia katika kipindi chote walichokuwa wanatekeleza majukumu yao.

Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Tanzania Mustapha Siyani, akizungumza baada ya hafla hiyo, alisema wananchi hawapaswi kuwa na wasiwasi na mahakama nchini, kwa kuwa mahakama ni huru, hivyo waendelee kuitumia.

Jaji Siyani alisema mahakama katika ngazi zote kuanzia kata, wilaya hadi Mahakama ya Rufani hakuna sababu ya kuwa na wasiwasi kwa sababu haki inapatikana mahakamani.

"Majaji hawa wanapoondoka wanaacha pengo, kama mlivyosikia majaji wenzao wakisifia umahiri kutoka kwao, sisi kama Mahakama Kuu ya Tanzania kila jaji ni muhimu na anapoondoka mmoja, pengo lazima litakuwapo. Ninachotumaini ni kwamba majaji wanaobakia watachukua mafunzo kutoka kwa majaji hawa watatu tuliowaaga kitaaluma," alisema Jaji Siyani.

## Spika Tulia amkaribisha Sugu wachuane, akiahidi kumfyeka

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya serikali kuweka wazi Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, ameshawasilisha hoja ya kuligawa Jimbo la Mbeya Mjini, Spika huyo ameibuka na kusema hana wasiwasi na Uchaguzi Mkuu ujao.

Amesema hata mpinzani wake katika Uchaguzi Mkuu uliopita, Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu, anaujua moto wake.

Spika Tulia alitoa kauli hiyo jana katika mazungumzo na kituo cha runinga, yaliyofanyika kwenye makazi rasmi ya Spika jijini Dodoma.

"Ninavyosema hivi kwamba majaliwa ya Mwenyezi Mungu, Inshaallah atuweke! Nipo vizuri wala sina wasiwasi juu ya hilo, hata yeye (Sugu) anajua.

"Hawa wanaojadili kwenye mitandao, wengine Mbeya hawajafika. Hawapajui! Wale watu wa Mbeya hawajawasikia.

"Mbeya mnakaribishwa, mkitawanyika kule msiseme mimi nina kamera sijui ni ahaaa! Wewe uliza hapa Mbeya Mjini mbunge nani? Mna mpango gani? Halafu utapata hiyo picha. Hata yeye (Sugu), moto wake anaujua," alitamba.

Akifafanua kuhusu hoja ya kuligawa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia alisema "uhalisia wenyewe ni hivi; jana (juzi) bungeni, aliyeuliza swali apewe sifa yake - Mheshimiwa Sophia Mwakagenda wa Viti Maalam. Aliuliza swali, tena la nyongeza. Si la msingi!"

Dk. Tulia ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alisema kuwa naibu waziri huyo alijibu kwamba serikali iko katika mchakato wa kuyatazama majimbo yote nchini kwa kuyaangalia yale ambayo ni makubwa, ili kuwasogezea wananchi huduma na uwakilishi.

"Kwa sababu wanapogawa jimbo na huduma zinaongezeka. Sasa hivi Jimbo la Mbeya Mjini lina kata 36. Kama likigawiwa, kata zingine zitakuwa jimbo hili na zingine, maana yake wabunge tutakuwa wawili. Ninasema tutakuwa kwa sababu nitakuwa mbunge," alisisitiza Dk. Tulia.

Hata hivyo, uteuzi wa wagombea ubunge kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 haujafanyika.

Spika huyo aliendelea: "Sasa ubunge wangu mimi haijalishi jimbo limegawanywa ama halijagawanywa. Mimi si ndio mbunge hivi sasa. Kama nilimtoa mtu kata zikiwa 36, yeye (Sugu) ataweza kunitoa kata zikiwa chache kweli? Jimbo kimsingi limejaa.

"Huu mchakato si wa Mbeya pekee. Nieleze wabunge wengi wanaodai majimbo si kwamba wameibuka tu, zipo sababu za msingi na msingi wa mgawanyo wa majimbo ni kuwasogezea wananchi huduma.

"Yale majimbo baada ya muda sifa zinavyoongezeka, yanakuwa halmashauri maana yake inakuwa na mkurugenzi wake, hivyo watu wanapata huduma kwa ukaribu," alisema.

Spika Tulia alisema hashangai kuona na kusikia anajadiliwa na anaamini inampa sifa fulani. Anafurahia kujadiliwa.

"Kama kuna mambo huwa ninafurahi ni kujadiliwa. Huwa ninapenda sana kujadiliwa, na wao wameanzisha huo mjadala. Mimi nimefurahi sana. Wanavyosema watanifuata, mimi ninataka wajipime.

Kama wanaona kina cha maji kinawatosha waje.

"Kama niliwatoa na kata 36, wataniweza wapi na kata chache? Zibaki 36 yaani ninawafyeka, sasa wewe unataka maendeleo ya wananchi wako halafu hutaki jimbo ligawanywe, wewe lazima una matatizo," alifafanua.

Alipoulizwa kuhusu hofu yake kukabiliana na Sugu katika uchaguzi ujao amba0 serikali imeahidi utakuwa huru na haki, pia imani ya upinzani dhidi ya mamlaka zinazosimamia uchaguzi, Spika Tulia alisema: "Hapana! Unajua umesema mwenyewe kwamba wanaamini. Sasa imani huwa inaambatana na hisia ambazo zinaweza kuwa na ukweli au hapana.

"Na imani hata vitabu vyetu vya dini huwezi kuamini kitu ulichokiona. Kwa mfano, sasa hivi huwezi kuwa na imani na nyumbani kwa Spika kunafananaje (yalikofanyika mazungumzo). Umeshafika yule mwenye picha kichwani ni ambaye hajafika," alieleza.

Spika alisema nchi imeweka utaratibu mzuri wa kikatiba na kisheria. Mtu akishaona ile imani yake imesimama kwenye kitu fulani, anapaswa kwenda mahakamani.

Spika Tulia pia alidai aliyoahidi jimboni Mbeya Mjini yametekelezwa kwa zaidi ya asilimia 100.

Juzi serikali ilibainisha kuwa Dk. Tulia ni miongoni mwa wabunge waliowasilisha hoja ya kutaka majimbo wanayoyawakilishwa yagawanywe kutokana na ukubwa na wingi wa wakazi, ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Ni kauli iliyoibua mjadala, ikiwamo katika vyombo vya habari kutokana na upinzani mkali uliopo kati ya CCM na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), pia ushindani kati ya Dk. Tulia na Sugu.

HABARI KITAIFA

# Wanafunzi wafa wakimsaidia fundi ujenzi ukuta wa shule

**Na Oscar Assenga,** LUSHOTO

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Msingi Shashui Kata ya Soni, Lushoto mkoani Tanga wamefariki dunia baada ya kuangukiwa na ukuta wa darasa.

Inadaiwa kuwa wanafunzi hao waliagizwa na mwalimu wamsaidie fundi kujenga ukuta wa darasa baada ya kuezuliwa paa.

Wanafunzi waliofariki dunia katika tukio hilo ni Salim Twahiru wa darasa la tatu na Abdallah Demadema wa darasa la nne mwenye umri wa miaka 10.

Akithibitisha kutokea kwa vifo hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Kalisti Lazaro, alisema mafundi walikuwa wanajenga madarasa matano, mawili yalikuwa yamevunjika na fundi alikuwa anavunja kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mapya.

Lazaro alisema wakati wakiendelea na uvunjaji huo, ukuta mmoja ulikuwa umebaki na ulidondoka, hivyo na kusababisha vifo wa wanafunzi hao.

Kutokana na tukio hilo, mkuu huyo wa wilaya alisema walimu wawili, akiwamo mwalimu mkuu wa shule hiyo, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano zaidi huku fundi naye akiisaidia polisi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bumbuli, George Haule, akizungumzia tukio hilo, alitoa pole kwa wazazi na walezi wakati walipopeleka miili ya wanafunzi hao katika Kituo cha Afya Bumbuli.

Machi 16, mwaka huu, mwanafunzi mmoja katika Shule ya Sekondari ya Mwinuko, Ilemela mkoani Mwanza alifariki dunia baada ya kudondokewa na jiwe wakati yeye na wanafunzi wenzake 30 wakitekeleza adhabu ya kuchimba changarawe kutokana na kuzungumza Kiswahili badala ya Kiingereza.

Mbali na mwanafunzi huyo, Glory Faustine (14) wa kidato cha kwanza kufariki dunia, mwingine Emmanuel Liatu (13) alivunjika mguu baada ya kudondokewa na jiwe katika shimo walilokuwa wakichimba changarawe.

Hatua hiyo ilisababisha Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kuwashikilia Mkuu wa Shule, Walu Steven, na aliyekuwa mwalimu wa zamu kwa mahojiano.



Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Apoteza maisha kwa kushambuliwa na tembo

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MZEE wa miaka 60 mkazi katika kijiji cha Mbati, Tunduru mkoani Ruvuma, Ally Mussa (60), amefariki dunia baada ya kishambuliwa na tembo.

Sambamba na mauaji hayo, pia zaidi ya tembo 30 wamevamia mashamba ya wakulima wa kijiji hicho yenye ukubwa wa ekari nne na kula mazao mbalimbali yakiwamo ya mdogo wa marehemu, Said Hemed.

Taarifa za tukio hilo zinaeleza kuwa Mussa aliuawa na tembo hao kwa kukanyagwa sehemu mbalimbali za mwili wake.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema katika tukio hilo, Mussa alivamiwa na kundi la tembo Aprili 23, mwaka huu, wakati akitoka shambani kurudi nyumbani.

Mjane wa marehemu, Sofia Mkwanda, alisema mume wake ameacha wake wawili, watoto 12 na wajukuu watatu.

Diwani wa Mbati, Rashid Swalehe, alikiri kutokea kwa matukio hayo likiwamo la Mussa kuuawa na tembo huku akisema makundi ya wanyamapori hao yameshamiri katika eneo hilo na wamekuwa wakisababisha madhara ya ulemavu wa maisha, vifo na kula na kufanya uharibifu wa mazao ya wananchi.

Kutokana na matukio hayo, diwani aliomba serikali kuongeza vifuta jasho kwa wananchi wanaouawa na kuharibiwa mazao pamoja na kifuta machozi kwa wananchi wanaojeruhiwa na wanyama hao.

Hata hivyo, diwani huyo aliwahamasisha wakulima kutumia teknolojia ya kuweka wigo wa pilipili iliyochanganywa na oili chafu kwenye mashamba yao ili kujikinga na wanyama hao.

Takwimu za matukio katika ofisi ya diwani huyo zinaonyesha kuwa takriban watu 15 waliripotia kufariki dunia kutoka na kuvamiwa na kushambuliwa na makundi ya tembo wakati wakifanya shughuli za kilimo katika makazi au mashamba tangu mwaka 2020 hadi sasa.

Aidha, takwimu hizo zinaonyesha kuwa katika kipindi hicho, wananchi 13 walijeruhiwa katika matukio hayo na kusababishiwa ulemavu wa kudumu.

# Sakata ununuzi Tanga Cement latikisa Bunge

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SAKATA la ununuzi wa hisa za kampuni ya saruji ya Tanga, jana lilitikisa Bunge huku likiwagawa wabunge, baadhi yao wakiunga mkono na wengine wakipinga vikali.

Tume ya Ushindani (FCC) iliidhinisha mapendekezo ya kutwaliwa kwa kampuni hiyo kwa Twiga Cement kukunua hisa lakini kwa masharti kuwa isifunge shughuli za Tanga Cement na kuzalisha saruji ya chapa ya Simba ambayo inazalishwa na kampuni hiyo.

Kutokana na uamuzi huo, baadhi ya wawekezaji katika uzalishaji wa saruji walipinga uamuzi huo katika Baraza la Ushindani wa Biashara (FCT) kwa madai kwamba kuruhusu muunganisho huo kungezuia ushindani au upangaji wa bei kwa kuwa Twiga atakuwa na udhibiti wa soko hivyo kuwapo kwa ukiritimba. Walidai kuwa hatua hiyo ni kinyume cha Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003.

Wadau waliopinga muunganiko huo wa Twiga na Tanga Cement ni Kampuni ya Saruji ya Chalinze na Chama cha Watetezi wa Watumiaji Tanzania (CAS) na hatimaye FCT ambayo ilitengua muunganisho huo katika uamuzi wake uliotolewa Septemba 23, 2022. Pamoja na uamuzi huo wa FCT, Februari, mwaka huu, FCC ilirejea na kutangaza muunganiko huo ambao pia umelalamikiwa na baadhi ya wadau wakiwamo wanasheria ambao mwishoni mwa wiki iliyopita walisema wanaiomba FCT kukazia uamuzi wake wa kuzuia mchakato huo kwa kukazia hukumu.

Wakichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2023/24, baadhi ya wabunge walipinga hatua ya uuzwaji wa hisa za kampuni hiyo na wengine wakitaka mchakato uendelee.

Mbunge wa Gairo (CCM), Ahmed Shabiby, alisema: "Mimi sioni shida mmiliki ambaye ana asilimia 68.8 anataka kuuza hisa zake. Shida iko wapi? Tunachotakiwa kukifanya ni kuhakikisha je, kiwanda kitafanya kazi baada ya kuuzwa? Wafanyakazi hawatapoteza ajira zao? Mtu anataka kuuza kitu chake mnampangia?"

Hata hivyo, hoja ya Shabiby iliombewa taarifa na Mbunge wa Bunda Vijijini, Mwita Getere, ambaye alisema Tanga Cement ni mali ya wananchi, hakitakiwi kuuzwa wala kubinafsishwa huku Mbunge wa Mkinga (CCM), Dunstan Kitandula, alisema wananchi wa Tanga ni waathirika wa uwekezaji kwamba waliwahi kugongwa na nyoka, hivyo wakiguswa na unyasi wanashtuka.

Alisema mwaka 2017 mwekezaji alijitokeza kuwekeza sekta ya saruji eneo la Mkinga na mwaka 2019 Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilimpatia leseni ya uwekezaji. Alisema mwaka 2020 mwekezaji huyo alianza kulipa fidia wananchi, baadhi wakaanza kuachia maeneo lakini wengine (wananchi 1,410 wanadai zaidi ya Sh. milioni 500 kama fidia.

"Hatutaki kuona Tanga Cement inataifishwa na kuwa gofu. Hii ndiyo hofu yetu wakazi wa Tanga. Tunachohitaji utaratibu ufanyike," alisema Kitandula.

Mbunge wa Korogwe Vijijini, Timotheo Mnzava, alisema muunganiko wa Twiga Cement na Tanga Cement ni kinyume cha Sheria ya Ushindani kifungu cha 11 (1).

Mnzava alisema licha ya sakata hilo kufikishwa FCT na kutolewa uamuzi wa kuzuiwa kwa mchakato huo, uamuzi huo umedharauliwa na kukiukwa jambo ambalo alisema linakiuka utawala wa sheria.

Alisema FCC ilidharau uamuzi wa mahakama na FCT ambacho ni chombo cha kisheria katika masuala ya ushindani wa biashara kwa kuendelea na mchakato wa muungano wa kampuni hizo jambo ambalo amesema, linazua maswali mengi.

"Desemba, 2022 kampuni ya Scancem (kampuni yenye hisa nyingi katika Twiga Cement) imeiandikia FCC kuomba kupewa kibali cha ya kuhamisha hisa za Afrisam (kampuni yenye hisa nyingi Tanga Cement) kwenda Scancem. Jambo hili linakwenda kinyume cha FCC.

"Hofu yetu ni kwamba Twiga Cement inapomchukua Tanga Cement, je, biashara itaendelea? Brand ya Tanga Cement itaendelea kuwapo?" Alihoji.

Pia alisema kuna hatari ya muungano huo kuwafanya kuwa wamiliki wakuu wa biashara ya saruji na pengine hata kupanga bei wanazozitaka na hata kuleta athari katika uchumi wetu.

Mbunge wa Viti Maalum, Judith Kapinga, alisema FCC imefanya utafiti kwamba kampuni hizo zikiunganishwa zitaimarisha soko na upatikanaji wa saruji kwa mikoa ya kaskazini asilimia 92, Kanda ya Ziwa asilimia 77, Pwani asilimia 60 na Kanda ya Kati asilimia 49. Pamoja na kutetea kuwa mchakato uwapo, alisema: "Hakuna mtu anayekataliwa kununua hisa ila tunachotaka utaratibu ufuatwe."

Endapo muunganiko huo utakubaliwa, Twiga Cement na Tanga Cement zitakuwa na 42.27 ya hisa zote za biashara ya saruji nchini, kitu ambacho kinatajwa kuwa ni kinyume na sheria ya ushindani.

HABARI KITAIFA

# RC ashtuka wenye fedha kunyanyasa wanawake

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aziagiza serikali za vijiji kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kukomesha vitendo vinavyofanywa na baadhi ya watu wenye fedha, kuwanyanyasa wanawake katika Wilaya ya Mkalama.

Akizungumza jana wakati akisikiliza kero za wananchi wa Kata ya Nkalakala wilayani Mkalama jana, kiongozi huyo alisema kuna uonevu mkubwa dhidi ya wanawake unaofanywa wenye fedha wilayani hapa, hasa kuwanyang'anya ardhi.

"Nilichogundua hapa Mkalama kinamama wanaonewa sana! Yaani mume wake akishafariki dunia, wanataka wamnyang'anye kila kitu. Hapana, haiwezekani! Niombe serikali za vijiji tuwatee na serikali za vijiji mkiwa tayari kuwatetea wanaoonewa, tutawashinda na katika hili TAKUKURU ninaomba wasaidie," aliagiza.

Serukamba alisema wanaotumia fedha zao, wakishajua serikali imekuwa na ukali wataacha kunyanyasa kinamama, hivyo kinachotakiwa ni serikali za vijiji kuanza kushughulika kukomesha vitendo hivyo.

Pia alikerwa na kitendo cha viongozi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Wilaya ya Mkalama kuruhusu zaidi ya Sh. milioni nne kurejeshwa makao makuu ilhali zilipaswa kutolewa kwa wananchi 32 waliopewa kazi ya kuchimba bwawa.

Fedha hizo zilirejeshwa makao makuu ya TASAF kwa kuwa siku ya malipo, wanufaika hawakuwapo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo ugonjwa. Wenyeviti wa vijiji wanavyotoka hawakuandika barua kuujulisha mfuko huo kuwa walengwa wanaumwa.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Mkalama, Goodluck Mlau, alikiri fedha hizo zilirejeshwa makao makuu kwa kuwa malipo ya TASAF huwa yanafanyika kwa siku moja tu na asiyekuwapo fungu lake linarejeshwa makao makuu.



Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Massala (wa pili kulia), akikabidhi vitendea kazi kwa mmoja wa wahitimu wa mradi wa KCB 2jiajiri, fundi uashi, Halima Chacha, wakati wa mahafali ya vijana 295 jijini Mwanza jana. Mradi huo, umewanufaisha vijana 960 nchini ni ubia wa Sh. bilioni 2.2 kati ya KCB Foundation na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ). Wengine ni Mkuu wa Chuo cha VETA, Lupakisyo Mapamba (kulia) na (wa pili kushoto) ni Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uhusiano wa KCB, Christine Manyenye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Viwanda vilivyobinafsishwa virudishwe'

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Viwanda na Biashara imeiagiza serikali kuvirudisha viwanda vilivyobinafsishwa na havijaendelezwa, kuwapatia wamiliki wengine ili vizalishe, kuongeza tija, ajira na mapato.

Imesema viwanda hivyo vinakiuka lengo la ubinafsishwaji na hivyo kulitia taifa hasara.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, David Kihenzile, aliyasema hayo jana bungeni alipowasilisha taarifa ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2023/24.

"Viwanda ambavyo vilibinafsishwa lakini mpaka sasa havifanyi kazi iliyokusudiwa, vinakiuka lengo la ubinafsishwaji wake na hivyo kulitia taifa hasara.

"Kamati inaishauri serikali kuvirudisha viwanda vyote vilivyobinafsishwa ambavyo havijaendelezwa na kuvitangaza upya kwa wamiliki wengine ili vizalishe na kuongeza tija, ajira na mapato," alisema.

**LIGANGA NA MCHUCHUMA**

Kihenzile pia alisema ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya kimkakati ikiwamo wa Liganga na Mchuchuma unapaswa kufanyika haraka.

Alisema kamati inaishauri serikali kuhakikisha wananchi wote ambao maeneo yao yanatwaliwa, walipwe fidia haraka kulingana na thamani ya ardhi yao.

Kihenzile alisema ulipaji wa fidia uende sambamba na mpango mkakati wa kuanza utekelezaji wa miradi hiyo ili kufikia lengo lililokusudiwa.

"Serikali ihakikishe kuwa mwekezaji katika mradi huu anarudisha fedha za fidia zinazolipwa na serikali wakati wa kuanza utekelezaji wa mradi kama mkataba wa makubaliano unavyosema," alisema Kihenzile.

**UCHUMI WA BULUU**

Kihenzile alisema kuna tatizo la kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa buluu, kwamba Tanzania haijaweka mkazo katika kukuza mazao yanayotokana na bahari, mito, maziwa na mabwawa.

Alisema kamati inaishauri serikali kujenga viwanda vikubwa vya kuchakata samaki na vya uzalishaji wa chakula cha samaki nchini.

Kihenzile alisema serikali inapaswa kuweka mikakati madhubuti ya kuuza samaki nje ya nchi na kudhibiti samaki kutoka nje ambao wanapatikana nchini wasiingie nchini.

**LESENI ZA BIASHARA**

Kihenzile ambaye ni Mbunge wa Mufindi Kusini (CCM), alisema kuwapo tatizo la wafanyabiashara kutakiwa kulipa kodi ya mauzo kabla ya kuanza biashara, kumeleta usumbufu kwa walipakodi na kuwakatisha tamaa.

Alisema kamati inaishauri serikali kuhakikisha vyombo husika vinatoza kodi kwa mujibu wa sheria na kupunguza urasimu katika mchakato wa kuanzisha biashara ili kuvutia wafanyabiashara wengi zaidi. Alisema elimu ya mlipakodi itolewe mara kwa mara kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima, wizara ijiwekee mikakati ya kukutana na wafanyabiashara kwa madaraja yao ili kusikiliza matatizo na kuyatatua.

**UINGIZAJI VYAKULA**

Kihenzile alisema suala la uingizaji wa bidhaa za chakula nchini limepata sura tofauti kutokana na hali ilivyo duniani, kwamba baadhi ya wafanyabiashara wamekosa uaminifu na kutengeneza vyakula visivyo salama.

Alisema hali hiyo inatishia usalama wa wananchi wetu, kwamba kamati inaishauri Shirika la Viwango Tanzania (TBS) iongezwe uwezo kifedha, rasilimali watu na vitendea kazi ili idhibiti bidhaa sizizo na ubora kuingia nchini.

Kihenzile alisema serikali iziwezeshe sekta za uzalishaji wa bidhaa za viwandani na mazao yatokanayo na kilimo nchini kuzalisha kwa wingi ili kujitosheleza kwa chakula na kupunguza uingizaji bidhaa hizo. Kihenzile alishauri: "Serikali ihakikishe bidhaa zote za chakula zinazoingizwa nchini zina ubora stahiki na usalama kwa walaji".

twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

**TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY**
**TAARIFA KWA WANAHISA**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa wote wa Tanzania Portland Cement Public Limited Company kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa utafanyika:

**Johari Rotana Hotel – Almasi Ballroom**
**Sokoine Drive, Dar-es-Salaam,**
**siku ya Jumatano, tarehe 31 Mei 2023, saa nne asubuhi.**

**DONDOO**

1. Ufunguzi wa Mkutano: Katibu kusoma taarifa iliyotolewa kuuita Mkutano Mkuu na kuhakiki kama akidi ya Mkutano imetimia.
2. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 30 uliofanyika tarehe 25 Mei 2022.
3. Kupokea, kujadili na kama zitaafikiwa kupitisha taarifa ya wakurugenzi, taarifa ya wakaguzi na taarifa ya fedha kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2022.
4. Kupokea, kujadili na kama litaafikiwa kuthibitisha gawio la mwaka 2022.
5. Kuthibitisha uteuzi wa wakaguzi wa mahesabu kwa mwaka unaoisha tarehe 31 Desemba 2023.
6. Kujadili mambo mengine ya kampuni ambayo taarifa zake zimepokelewa.

**Kwa Niaba ya Bodi**
**Tarehe: 5 Mei, 2023**

**Katibu wa Kampuni**

1. Mwanahisa yeyote aliye na haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano, anaruhusiwa kuteua mwakilishi au wawakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake. Fomu ya kuteua mwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya kampuni (https://www.twigacement.com).
2. Mwakilishi atakayeteuliwa siyo lazima awe mwanahisa wa kampuni. Fomu ya kuteua mwakilishi ambayo imejazwa na mwanahisa inatakiwa iwasilishwe kwenye ofisi za kampuni, Wazo Hill, Dar es Salaam angalau masaa 24 kabla ya muda wa kuanza mkutano, la sivyo fomu itakuwa haijakidhi vigezo.
3. Kwa ajili ya utambulisho, mwanahisa anatakiwa kuja na cheti cha umiliki wa hisa pamoja na kitambulisho chake (pasi ya kusafiria, leseni ya udereva, au kitambulisho cha taifa, cha kazi, au cha mpiga kura).
4. Mahesabu kamili ya kampuni, ambayo yamepitishwa na wakaguzi, yanapatikana kwenye ofisi za kampuni, Wazo Hill, Dar es Salaam, au pia kupitia tovuti ya kampuni **(https://www.twigacement.com).**

# Miradi mipya 240 uwekezaji yasajiliwa

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

KATIKA kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, mwaka huu, serikali imesajili miradi mipya 240 inayotarajiwa kuwekeza Sh. trilioni 10.2, pamoja na kutengeneza ajira 39,245.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa wizara yake kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema serikali imeendelea na juhudi za kuhamasisha na kuvutia uwekezaji nchini pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara.

Dk. Kijaji alisema kati ya miradi hiyo ya wazawa ni 89, wageni 94 na ubia 57, ikiwa ni ongezeko la miradi 34 sawa na asilimia 16.5 ikilinganishwa na ongezeko la miradi 34 iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

Alisema kati ya miradi 240 iliyosajiliwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, miradi 187 sawa na asilimia 77.9 imeanza utekelezaji kwenye sekta za kilimo (18), majengo ya biashara (10), miundombinu (2), rasilimali watu (5), viwanda (101), huduma (5), mawasiliano (1), utalii (9) na usafirishaji (36).

Kijaji alisema tathmini inaonyesha kuwa idadi ya miradi iliyosajiliwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 katika mabano iko katika sekta za uzalishaji viwandani (1040, usafirishaji (56), kilimo (180, ujenzi wa majengo ya biashara (22), utalii (21), huduma (130, miundombinu (mitatu) na rasilimali watu (mitatu).

Alisema katika miradi iliyosajiliwa katika kipindi hicho sekta ya uzalishaji viwandani inaongoza kwa kuwa na mtaji mkubwa wa Dola za Marekani bilioni 2.80 ikifuatiwa na sekta ya usafirishaji yenye mtaji wa Dola za Marekani milioni 861.95, sekta ya ujenzi wa majengo ya biashara inafuata ikiwa na mtaji wa Dola za Marekani milioni 382.45.

Aidha, alisema sehemu kubwa ya miradi iliyosajiliwa katika kipindi hicho inatarajiwa kuwekezwa katika mikoa ya Dar es Salaam miradi 111, Pwani (33), Mwanza (12), Arusha (12) na Dodoma (11).

Dk. Kijaji alisema hali hiyo imechangiwa na uwapo wa masoko na miundombinu wezeshi kama vile umeme, maji, barabara, bandari na viwanja vya ndege katika mikoa hiyo.

Kadhalika, alisema katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023 wizara imesajili miradi mitano katika maeneo maalum kwa mauzo nje ya Dola za Marekani milioni 15.6.

Alisema miradi hiyo inatarajiwa kuchangia mauzo ya nje yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 12.46 na kutoa ajira kwa Watanzania 1,247.

# ACT yadai doria baharini na ziwani zinachochea rushwa

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimedai doria baharini na ziwani zinazoendeshwa kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu, zimegeuka vyanzo vya rushwa.

Kimesema doria hizo zimegeuka kuwa kero kwa wavuvi na kusababisha mianya ya rushwa miongoni mwa maofisa uvuvi nchini.

Waziri Kivuli wa Kilimo, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi wa chama hicho, Mtutura Mtutura, alidai hayo jana mkoani Dar es Salaam alipozungumzia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2023/24.

"Doria hizi zimekuwa zikiwakumba mpaka wanunuzi wa samaki kwa lengo la kitoweo. Pamoja na nia njema ya kuepukana na uvuvi kwa njia haramu zinazoangamiza samaki na mazalia yake, ACT-Wazalendo tusichounga mkono, ni doria kugeuka kero.

"Zinasababisha mianya ya rushwa kwa maofisa uvuvi nchini. Doria hizi zinaendeshwa kama njia ya kujipatia kipato cha ziada maofisa wa idara ya uvuvi," alidai.

Alisema kuwa kwa sasa kuna utaratibu umeanzishwa na maofisa uvuvi wa kuwataka wavuvi wasio na leseni ya uvuvi, wachange fedha na kuwakabidhi ili wawaruhusu kufanya uvuvi, akidai wasipofanya hivyo hupita doria kali inayokamata vifaa vyao na kuviteketeza na kuwapiga faini kubwa.

"Licha ya Bunge kupitisha makadirio haya, bado ipo fursa ya kuendelea kujadiliana kwa wakati uliopo. Yapo mambo yanaweza kufanyiwa marekebisho madogo ili kuhakikisha mpango na bajeti unaakisi mahitaji ya wananchi," alisema.

Mbali na hilo, Mtutura pia alisema wamebaini ukamataji wa mifugo maeneo ya hifadhi unaambatana na unyanyasaji kwa wafugaji, akidai baadhi ya askari -pori hutumia kisingizio cha wafugaji kuvamia maeneo ya hifadhi kufanya ukatili huo.

"Pamoja na kutenga maeneo ya hifadhi na maeneo ya malisho, bado kumekuwa na ukamatwaji holela wa mifugo na utozwaji wa faini kubwa kinyume cha sheria za nchi.

"Kumekuwa na tabia endelevu ya askari wa maliasili kuvamia wafugaji na kutaifisha mifugo yao kisha kuiuza kinyemela pasi na kufuata kanuni za mauzo ya minada kwa mali zinazotaifishwa, kupigwa risasi au kuwatoza faini kubwa kinyume cha sheria. Katika siku za hivi karibuni kumekuwa na manung'uniko makubwa kwa wafugaji wa Wilaya ya Kaliua," alisema.

Waziri kivuli huyo alisema ACT-Wazalendo inatoa wito kwa taasisi za umma, hasa mamlaka za hifadhi kuacha mara moja uonevu na unyang'anyi na kufuata sheria, ili wafugaji waendeshe shughuli zao kwa uhuru na amani.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

AUDITED RESULTS FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2022

STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME
FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2022

| TZS '000 | 2022 | 2021 |
|---|---|---|
| Revenue from contracts with customers | 494,716,182 | 449,509,301 |
| Cost of sales | (328,592,344) | (293,185,036) |
| Gross profit | 166,123,838 | 156,324,265 |
| | | |
| Other operating income | 841,677 | 1,205,920 |
| Selling and marketing expenses | (3,082,702) | (3,010,835) |
| Administrative expenses | (25,216,626) | (23,514,168) |
| Other operating expenses | (2,727,675) | (5,423,601) |
| Operating profit | 135,938,512 | 125,581,581 |
| | | |
| Finance income | 3,139,579 | 3,258,481 |
| Finance costs | (810,519) | (611,279) |
| Net gain/ (loss) on foreign currency translation | 1,829,994 | (191,595) |
| Profit before tax | 140,097,566 | 128,037,188 |
| | | |
| Income tax expense | (42,738,964) | (39,555,603) |
| Profit for the year | 97,358,602 | 88,481,585 |
| | | |
| Other comprehensive income | | |
| Other comprehensive income not to be reclassified to profit or loss in subsequent periods: | | |
| Re-measurement gains/ (losses) on defined benefit plan | 448,834 | (1,538,346) |
| Income tax effect | (134,650) | 461,504 |
| Other comprehensive income/ (loss) for the year, net of tax | 314,184 | (1,076,842) |
| | | |
| Total comprehensive income for the year, net of tax | 97,672,786 | 87,404,743 |
| | | |
| Earnings per share | | |

CHAIRMAN'S STATEMENT

Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) continues to deliver strong operating results when compared to year 2021. Both the sales volume and revenue reached a record high compared to year 2021. Sales volume and revenue increased by 5% and 10% respectively.

This increase is due to the continued increased demand of cement products within Tanzania and outside Tanzania. The high availability and efficiency of the plant and machinery has contributed to the improved performance compared to year 2021, all within an environment where the Health and Safety of our employees and contractors is paramount.

The Company continues to focus on delivering excellent customer service, selling of high quality products and maintaining strong customer relationships to enable TPCPLC to demonstrate its strength as the leading player in the industry.

Prospects
The cement demand in Tanzania and in the East-African region has been growing steadily in recent years. TPCPLC is well placed to meet this growing demand and will continue to work on improving effi ciency and operating performance.

Dividend
The Board proposes a dividend for year 2022 of TZS 390 per share. The Register of Members will close on 29 May 2023, and the last day of trading cum dividend will be 24 May 2023. The dividend will be paid on or about 30 June 2023.

Appreciation
The Board would like to thank all its stakeholders for their support. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders and community in the future.

BY ORDER OF THE BOARD
Hakan Gurdal
Chairman of the Board

STATEMENT OF FINANCIAL POSITION
AS AT 31 DECEMBER 2022

| TZS '000 | 2022 | 2021 |
|---|---|---|
| ASSETS | | |
| Non-current assets | | |
| Property, plant and equipment | 142,330,100 | 144,842,101 |
| Intangible assets | 813,318 | 1,006,537 |
| Leasehold land | 980,929 | 1,008,775 |
| Right of Use assets | 4,333,991 | 982,483 |
| Other financial assets | 574,000 | 796,000 |
| | 149,032,338 | 148,635,896 |
| Current assets | | |
| Inventories | 85,992,840 | 52,935,488 |
| Trade receivables | 53,561,114 | 46,277,317 |
| Other short-term operating receivables | 24,193,735 | 16,586,868 |
| Other financial assets | 600,000 | 600,000 |
| Cash and cash equivalent | 105,512,644 | 114,278,364 |
| | 269,860,333 | 230,678,037 |
| | | |
| TOTAL ASSETS | 418,892,671 | 379,313,933 |
| | | |
| EQUITY AND LIABILITIES | | |
| Equity | | |
| Authorised, issued and fully paid-up share capital | 3,598,462 | 3,598,462 |
| Retained earnings | 296,139,811 | 268,637,039 |
| TOTAL EQUITY | 299,738,273 | 272,235,501 |
| | | |
| Non-current liabilities | | |
| Lease liabilities | 1,149,572 | 186,758 |
| Employment benefit liabilities | 5,339,322 | 5,306,943 |
| Provision for quarry site restoration | 4,266,311 | 2,432,541 |
| Deferred income tax liability | 10,066,585 | 11,618,859 |
| | 20,821,790 | 19,545,101 |
| Current liabilities | | |
| Lease liabilities | 3,461,375 | 1,044,405 |
| Current income tax payable | 521,690 | 28,859 |
| Trade and other payables | 91,444,170 | 83,611,599 |
| Dividend payable | 2,905,373 | 2,848,468 |
| | 98,332,608 | 87,533,331 |
| TOTAL LIABILITIES | 119,154,398 | 107,078,432 |
| TOTAL EQUITY AND LIABILITIES | 418,892,671 | 379,313,933 |

FINANCIAL STATEMENTS
FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2022

STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY

| | Share Capital and Share Premium TZS '000 | Retained earnings TZS '000 | Total Equity TZS '000 |
|---|---|---|---|
| As at 01 January 2022 | 3,598,462 | 268,637,039 | 272,235,501 |
| Profit for the year | - | 97,358,602 | 97,358,602 |
| Other comprehensive income, net of tax | - | 314,184 | 314,184 |
| | | | |
| Total comprehensive income, net of tax for the year | - | 97,672,786 | 97,672,786 |
| | | | |
| Transactions with owners in their capacity as owners: | | | |
| Dividends | - | (70,170,014) | (70,170,014) |
| As at 31 December 2022 | 3,598,462 | 296,139,811 | 299,738,273 |
| | | | |
| As at 01 January 2021 | 3,598,462 | 251,402,305 | 255,000,767 |
| Profit for the year | - | 88,481,585 | 88,481,585 |
| Other comprehensive loss, net of tax | - | (1,076,842) | (1,076,842) |
| | | | |
| Total comprehensive income, net of tax for the year | - | 87,404,743 | 87,404,743 |
| | | | |
| Transactions with owners in their capacity as owners: | | | |
| As at 31 December 2021 | 3,598,462 | 268,637,039 | 272,235,501 |

STATEMENT OF CASH FLOWS

| TZS '000 | 2022 | 2021 |
|---|---|---|
| Operating activities | | |
| Profit before tax | 140,097,566 | 128,037,188 |
| | | |
| Adjustment to reconcile profit before tax to net cash flows: | | |
| Depreciation and amortisation | 20,645,407 | 18,666,314 |
| Interest expense | 1,255,581 | 1,040,904 |
| Interest income | (3,139,579) | (3,258,481) |
| Net unrealised exchange loss | 801,765 | (620,896) |
| Net provision for slow moving and obsolete inventories | 971,658 | 2,058,943 |
| Increase in site restoration provision | 1,833,770 | 157,519 |
| Post-employment benefit provision | 300,810 | 226,950 |
| Expected credit losses for trade receivables | (339,944) | (421,078) |
| Gain on disposal of property, plant and equipment | - | (46,610) |
| Cash flows before changes in working capital items | 162,427,034 | 145,840,753 |
| | | |
| Working capital adjustments: | | |
| Increase in inventories | (34,029,010) | (2,589,649) |
| Increase in trade receivables | (6,943,853) | (4,765,323) |
| Increase in other short-term operating receivables | (7,606,944) | (2,105,812) |
| Decrease in other financial assets | 222,000 | 550,000 |
| Increase in trade and other payables | 7,832,570 | 14,851,403 |
| Corporation tax paid | (43,932,977) | (42,733,839) |
| Payment to post-employment benefit - Benefit payments | (264,659) | (950,058) |
| Interest received | 3,139,579 | 3,253,460 |
| Net cash inflows from operating activities | 80,843,740 | 111,350,935 |
| | | |
| Investing activities | | |
| Proceeds from disposal of property, plant and equipment | - | 46,610 |
| Payment for capital works-in-progress | (14,611,038) | (27,080,581) |
| Net cash flows used in investing activities | (14,611,038) | (27,033,971) |
| | | |
| Financing activities | | |
| Dividends paid | (70,113,111) | (70,178,005) |
| Payment of liabilities - principal and interest | (4,083,546) | (4,337,262) |
| Net cash flows used in financing activities | (74,196,657) | 74,515,267) |
| | | |
| Net (decrease)/increase in cash and cash equivalents | (7,963,955) | 9,801,697 |
| Net foreign exchange difference - unrealised | (801,765) | 620,896 |
| Cash and cash equivalents at 01 January | 114,278,364 | 103,855,771 |
| | | |
| Cash and cash equivalent at 31 December | 105,512,644 | 114,278,364 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usafiri wa usiku ni mzuri tathmini ifanyike kwanza

**KWA** muda mrefu, wadau mbalimbali wa usafirishaji wamekuwa wakiiomba Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), kurejesha utaratibu wa mabasi ya abiria mikoani kusafiri usiku kama ilivyokuwa zamani.

Serikali ilisitisha usafiri wa mabasi usiku mwaka 1992 baada ya ajali kuwa nyingi huku sababu kubwa ikielezwa kuwa ni uzembe wa madereva kutokana na kupata usingizi wakiwa wanaendesha vyombo hivyo. Pamoja na kwamba utaratibu huo wa mabasi ulisitishwa, yako yanayofanya safari hizo kati ya Dar es Salaam na Mbeya.

Katika maombi hayo, wadau hao wamekuwa wakiomba utaratibu huo urejewe huku wakisisitiza kuwa watakuwa makini katika kuwadhibiti madereva kwa kuwapa zamu pamoja na kuhakikisha vyombo hivyo vinakuwa na usalama kwa abiria wao.

Hata hivyo, LATRA imetoa tamko kuwa haijazuia mabasi kusafiri saa 24 isipokuwa kinachofanyika ni kuchukua tahadhari na kujiridhisha na hali ya kiusalama kabla ya kufikia hatua hiyo. Taarifa ya LATRA ilitolewa jana zikiwa siku chache tangu ilipotangaza kuruhusu magari yanayofanya safari mikoa ya Kigoma na Katavi kuanza safari saa 9.00 usiku.

Kwa mujibu wa mamlaka hiyo, baada ya kupokea ushauri kutoka kwa wadau, itaanza kuruhusu magari kuanza safari muda huo. Hata hivyo utaratibu huo bado unapingwa na TABOA ambayo inataka mabasi yaruhusiwe kuanza safari muda wowote, kwa kuwa kitendo cha mamlaka hiyo kuendelea kuyazuia ni kuchelewesha maendeleo.

LATRA katika kuweka sawa jambo hilo, imesisitiza kuwa kuruhusu mabasi kuanza saa 9:00 usiku, ni sehemu ya mwendelezo wa kuboresha usafiri wa mabasi baada ya awali kuruhusu mabasi kuanza safari saa 11:00 alfajiri na kwamba mabasi 180 yalishapewa ratiba.

Mamlaka pia imesisitiza kuwa licha ya kuruhusu muda zaidi, bado inaendelea kuangalia tahadhari za kiusalama ili kuona ni namna gani maafa yanaweza kudhibitiwa.

Suala la kuruhusu mabasi kusafiri saa 24 ni zuri kwa sababu linaweza kuwafanya baadhi ya abiria hasa wafanyabiashara kupata nafasi ya kupunguza muda wa safari na kufanya shughuli zao.

Kwa mfano, mfanyabiashara anayetoka Iringa, kama ataanza safari saa 9:00 usiku, anaweza kufika Dar es Salaam mapema na kufanya baadhi ya shughuli siku hiyo na hatimaye kurejea siku inayofuata.

Hata hivyo, kabla ya kufikia uamuzi huo, mambo kadhaa yanatakiwa kufanyiwa kazi yakiwamo usalama wa vyombo husika, hali ya madereva kuhimili muda wa kusafiri kwa maana kwamba wawe na afya na utimamu wa mwili.


Sambamba na hilo, tathmini ya kina inapaswa kufanyika ili kuona kama sababu zilizofanya kupigwa marufuku usafiri wa usiku haziko tena.

Ni vyema LATRA na wadau wa usafirishaji wakiwamo TABOA, wakakaa pamoja na kufikia makubaliano badala ya sasa kuendelea kuvutana.

LATRA na TABOA hawana budi kutambua kuwa wanajenga nyumba moja, hivyo hawana sababu ya kugombania fito. Lengo baina ya taasisi hizo liwe kuboresha usafiri na kuweka mbele maslahi ya abiria badala ya biashara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Beatrice Moses

## Muungwana Lazima Nilonge

# Huduma mwendokasi Barabara Morogoro ina shida, wenye dhamana liangalieni hilo

**USAFIRI** ni miongoni mwa huduma nyeti kwenye maisha ya kila siku ndani ya jamii, kwa kuwa unatumika kuwafikisha watu kutoka sehemu moja kwenda mahali pengine kulingana na shughuli husika, pia kufanya dhima tajwa ifikiwe.

Mfumo wa usafiri wa mabasi ya mwendokasi Dar es Salaam, ilianza kazi mkoani Dar es Salaam, mnamo tarehe 10 ya mwezi Oktoba, mwaka 2016, ikianza vituo vya Kimara na Morocco kwenda Kivukoni na Gerezani.

Kabla ya mradi huo kuanza, wakazi wa maeneo hayo walikuwa wakitumia usafiri wa daladala pekee, ambao katika ukweli ulikuwa ni changamoto kubwa, licha ya kuwa mabasi yaliyotumika yalionekana madogo, mengi yalikuwa aina ya Toyota Coaster, watu wanasongamana 'hivyo hivyo' ili mradi wafike wanakoelekea, pia wakikumbana na foleni.

Hivyo, kuanzishwa kwa huduma ya mabasi ya mwendokasi, kuliaminika kutasaidia kupunguza kero iliyokuwapo ikiwakabili wakazi wa maeneo, hasa kulikoshuhudiwa adha ya foleni kubwa.

Lakini, jambo la kushangaza ni kwamba huduma hiyo ilipoanza mabasi, yalijaza abiria, licha ya kuelezwa kuna jumla ya mabasi 140 yanayohudumia. Hilo likawashangaza wengi kwa jinsi huduma hiyo ilivyokuwa iktolewa, kwa kuwa ilitokea abiria kukaa kituoni zaidi ya dakika 20, bila basi kufika la kuwasafirisha!

Upandaji mabasi hayo ulikuwa wa kibabe na kutokana na wingi wa abiria vituoni, ilikuwa siyo ajabu kukuta abiria akiwa amedondoka na kukanyagwa na wenzake au kupoteza vitu mbalimbali, vikiwamo saa, hereni viatu na simu za mkononi.

Hali hiyo ilizua malalamiko mengi, baadhi walijikuta wakipata majeraha kisa usafiri wa mwendokasi. Wanafunzi nao walijikuta kwenye wakati mgumu, kwa kuwa walifika shuleni wakiwa wamechafuka, kutokana na kukanyagwa hasa wanaovaa soksi nyeupe.

Suala la kupanda kwenye mabasi hayo kwa ustaarabu kwa sasa, linaonekana kufanikiwa kwa kiasi fulani kwenye baadhi ya vituo hasa vituo vikuu ambapo utaratibu umewekwa wa kupanda kwa kujipanga kwenye foleni.

Nimesema 'kwa kiasi fulani' kwa kuwa, kuna baadhi ya abiria wamekuwa wakitumia vibaya nafasi za wagonjwa, wenye ulemavu na wazee hujipenyeza huko mara kadhaa. Nimewahi kushuhudia askari wakirushiwa lawama na abiria waliopo kwenye foleni, kuhusu kuvunjwa kwa utaratibu.

Wakati huu wa msimu wa mvua kuna vituo kadhaa havina majengo, abiria wanabaki wanateseka na wapo wanaoloweshwa na mvua, wakati wakisubiri mabasi ya mwendokasi kwenye vituo hivyo. Huja kwa vielelezo! Nikitumia mfano ninaoushuhudia katika Barabara ya Morogoro, kuanzia eneo la Kimara Stop Over, Suka, Temboni hadi Mbezi kwa Msuguri na Kibanda cha Mkaa pamoja na vinavyofuatia, hadi kufika Kibaha, abiria wanataabika hasa inapotokea ajali au msafara wa viongozi, huwa wanasimama muda mrefu vituoni, licha ya kwamba miongoni mwao kuna wagonjwa, wazee na wajawazito, hakuna hata 'benchi ' la kukaa.

Hapo pia niwataje katika kundi hilo kuna wanafunzi ambao suala la muda kwao ni muhimu sana, kama ilivyo kwa wakubwa wao wanaoenda kwenye maeneo ya biashara, hali kadhalika kazi mbalimbali.

Ni wazi kwamba ujenzi wa barabara katika maeneo hayo haujakamilika, lakini kuna ujenzi wa vibanda vya ofisi za kukatia tiketi ulifanyika kwenye maeneo hayo, ambao ungeweza kuendana na hekima iwapo mahali hapo pa kuwapumzisha wagonjwa, wajawazito na wahitaji wengineo. Ajabu ni kwamba, kuna marufuku imewekwa ya kuzuia kupiga picha katika maeneo ya vituo vya mwendo kasi hali ambayo inazua maswali mengi ikiwamo je, hatua hii inalenga kuficha huduma mbovu zinazolalamikiwa?

Ifahamike kwamba, huduma ya mwendokasi ni mpya nchini, hivyo inachukuliwa kama kivutio kwa kiasi fulani, (utalii usio rasmi) hivyo baadhi ya abiria hutamani kuwa na kumbukumbu ya kupiga picha katika maeneo yake, lakini wanajikuta wakishambuliwa na walinzi wa vituo hivyo mara wanapobainika.

Hapo inashangaza kidogo, shida mahali hapo iko wapi? Kuna vigezo vipo vya usalama wa namna yoyote dhidi ya rasilimali hiyo, ambayo ni makali ya Mtanzania anayepiga picha au hata ikiwa kwa asiye Mtanzania. Pengine ni vyema viongozi wakalitazama vyema jambo hili, pia wakajitahidi kuwajibika ipasavyo katika kuboresha huduma kwenye mwendo kasi, iendane na makusudio yaliyowekwa na serikali na ikidhi matarajio ya watumiaji wa usafiri huo.

HABARI KITAIFA

# Sheria kali ya usalama barabarani yaandaliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imesema ipo mbioni kukamilisha marekebisho ya mapitio ya Sheria ya Usalama Barabarani ili iwe na makali.

Naibu Waziri wake, Jumanne Sagini, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Janeth Massaburi.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itafanyia maboresho sheria hiyo ili iwe kali na kudhibiti ajali za barabarani.

"Kuna nchi zina sheria kali za kudhibiti ajali na wanatii sheria kunusuru maisha ya wananchi wao. Lini serikali itatunga sheria kali ili kusaidia kunusuru maisha ya Watanzania yanayopotea kwa ajali za barabarani? Je, serikali imeshindwa kuwadhibiti madereva bodaboda ambao hupita kwenye makutano bila kuzingatia taa za barabarani na kusababisha ajali?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Sagini alisema serikali ilishawasilisha bungeni muswada wa sheria na ulishasomwa kwa mara ya kwanza na Bunge liliona irudishwe ili kuboresha maeneo yaliyobainika kuwa na kikwazo.

"Uboreshaji upo hatua za mwisho na katika mabunge yajayo ili iletwe na bunge likimaliza kupitisha tutakuwa tumemaliza eneo la sheria kali," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema serikali haijashindwa kudhibiti bodaboda na kwa sasa wanapatiwa elimu kwa kuwa wengi wao walikuwa hawajui taratibu za usalama barabarani.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji serikali haioni haja ya kuwapeleka maofisa wa usalama barabarani nchi za nje kama Falme za Kiarabu na Vietnam kujifunza jinsi ya kudhibiti ajali.

Sagini akijibu swali hilo, alisema serikali inao utaratibu wa kutoa mafunzo mbalimbali kwa maofisa wa polisi wa usalama barabarani ndani ya nchi na pia kuwapeleka nje ya nchi kujifunza namna bora ya kusimamia na kudhibiti ajali za barabarani.

"Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2023, serikali imeshawapeleka maofisa wa usalama barabarani 30 kwenye nchi 15 ambazo ni Marekani, Ujerumani, Japan, China ,India, Vietnam, Australia, Switzerland, Falme za Kiarabu, Israel, Tunisia, Misri, Ghana, Rwanda na Afrika Kusini ili kujifunza masuala ya usalama barabarani," alisema.

Pia alisema serikali itaendelea kutoa nafasi za mafunzo ndani na nje ya nchi kwa maofisa wa usalama barabarani ili kupata ujuzi juu ya usimamizi na udhibiti wa ajali.



Mkurugenzi wa Udhibiti Uchumi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Daniel Malanga (kushoto), akizungumza wakati wa kufungua mkutano mkuu wa mwaka wa viongozi wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE), Tawi la TCAA, mjini Morogoro hivi karibuni. **PICHA: DICKSON MULASHANI**

# 'Makandarasi wa ndani watumie wataalamu wenye sifa serikalini'

**Na Mary Geofrey**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, amewataka makandarasi wa ndani kutumia wataalamu wenye sifa kutekeleza shughuli zao ili kukidhi vigezo vinavyohitajika serikalini katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kupunguza matumizi ya makandarasi wa nje katika miradi mikubwa.

Jijini Arusha, Kasekenya alitoa kauli hiyo alipofungua Mkutano wa Tatu wa Kikanda wa Kushauriana na Wadau wa Sekta ya Ujenzi kwa Mwaka 2023, ulioandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kwa wadau wa ujenzi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Kasekenya alisema serikali inatoa kipaumbele kwa taasisi binafsi hususani katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.


"Serikali kupitia taasisi kama Wakala wa Majengo (TBA), Shirika la Reli (TRC) na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mkakati wa namna ya kushirikiana na sekta binafsi kutekeleza majukumu yao.

"Mfano tu ukikamilika mradi wa SGR (reli ya kisasa) , kutakuwa na vipande vitakavyokuwa vinafanyiwa ukarabati na sekta binafsi badala ya TRC wenyewe," alisema Kasekenya.

Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Joseph Nyamhanga, aliishukuru serikali kwa kupunguza matumizi ya 'force account' katika utekelezaji wa miradi yake.

Mkutano huo unawakutanisha makandarasi kutoka mikoa sita ya kaskazini na mikoa jirani ikiwamo Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Singida na Dodoma ambao wanajadili na kuweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha sekta ya makandarasi nchini.

**KABWELA** — Na Fadhili Mohammed



# Spika awaonya wabunge wanaodaiwa kodi na TBA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amewaagiza wabunge wanaodaiwa kodi ya pango na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kulipa madeni yao kabla hawajaanza kufukuzwa.

Dk. Tulia alitoa angalizo hilo jana bungeni wakati wa kipindi cha Maswali baada ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Asha Juma kuuliza swali la nyongeza. Mbunge huyo alisema nyumba nyingi za TBA Dodoma ni chakavu na kuhoji mpango wa serikali kusimamia nyumba hizo zikarabatiwe kwa kuwa wanaoishi wanalipa kodi. Hawakai bure.

Kutokana na swali hilo, Spika alisema: "Mbunge amezungumzia suala la hawakai bure. Wabunge wengi wanadaiwa na TBA. Wabunge mnaodaiwa kodi na TBA ilipeni TBA ili ifanye majukumu yake.

"Ninasema hivyo kwa sababu nina barua zenu. Itakapofika muda wa kufukuzwa huko kwenye majumba, msinifuate mimi. Nendeni mkalipe ili TBA ifanye kazi zake."

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, akijibu swali la mbunge huyo, alikiri baadhi ya nyumba za TBA Dodoma kuwa na uchakavu na kumshukuru Spika kwa kukumbusha wadai na watumishi wa serikali baadhi wanadaiwa.

"Kuna kila sababu ya kulipa ili kukarabati nyumba hizi chakavu, ikizingatiwa TBA fedha inazopata ni kutoka ruzuku ya serikali na fedha za kodi za pango zikikusanywa ndio zinakarabatiwa," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Chaani (CCM), Usonge Hamad Juma, alihoji mpango wa serikali kuwajengea nyumba watumishi wa Serikali ya Muungano kwa upande wa Zanzibar kupitia TBA.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mwakibete alisema TBA ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala, Sura 245 ikisomwa pamoja na agizo la uanzishwaji wa wakala la Februari 14, 2003.

"Moja ya jukumu la msingi la TBA ni kujenga na kukarabati nyumba na majengo ya serikali kwa ajili ya makazi kwa watumishi wa umma Tanzania Bara," alisema.

Hata hivyo, alisema jukumu la ujenzi wa nyumba kwa watumishi wa umma kwa upande wa Zanzibar liko chini ya Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA). TBA na ZBA wanashirikiana na kushauriana kwenye mambo mbalimbali ya kitaalamu na kujengeana uwezo.



Bibi mkazi wa kata ya Mitumbati, wilayani Nachingwea, mkoani Lindi, akieleza kero yake kwa Mkuu wa wilaya hiyo, Mohamed Moyo (kulia), wakati wa mkutano wa hadhara na wananchi katika ziara yake ya "Ulipo nipo toa kero yako sema kweli siyo majungu", katika vijiji vya Ntila, Maziwa, Mshikamano na Mitumbati juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ataka uadilifu ukaguzi wa mazingira migodini

**Na Robert Hokororo,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Dk. Switbert Mkama, amewataka maofisa mazingira na wakaguzi wa migodi kuwa waadilifu ili kutimiza azma ya serikali ya kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Alitoa rai hiyo juzi alipofungua warsha ya siku mbili kwa Maofisa Mazingira na Wakaguzi wa Migodi kuhusu Mikataba ya Minamata na Basel kwa ajili ya kupunguza matumizi ya zebaki iliyoanza juzi jijini hapa.

Dk. Mkama alisema Tanzania ilitia saini Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki Oktoba 10, 2013 kwa lengo la kupunguza matumizi ya kemikali hiyo yenye athari kwa afya na mazingira.

Aliwataka wakaguzi kuwa waadilifu katika shughuli zao kwa kuwa bila uadilifu, nchi itarudi nyuma katika kupunguza matumizi ya zebaki.

"Ninawaomba epukeni kuchanganya maslahi binafsi na ukaguzi ili kuhakikisha afya na mazingira yanakuwa salama na tutambue zebaki ina athari kiafya na mazingira," aliagiza.

Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Utunzaji wa Mazingira wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usamamizi wa Mazingira (NEMC), Redempta Samuel, alisema mafunzo hayo yatawajengea uwezo wa kutatua changamoto za kimazingira.

Alisema shughuli nyingi za uchimbaji mdogo wa dhahabu zinafanyika katika maeneo ya vyanzo vya maji na misitu na kuhusisha uharibifu wa mazingira, hivyo warsha itawapa uelewa kukabiliana na changamoto hizo.

Lucas Maselo kutoka Tume ya Taifa ya Madini, alisema mafunzo yatawajengea uwezo wa kuanza kuchagiza matumizi ya teknolojia ya kisasa ya uchenjuaji wa dhahabu badala ya zebaki.

Alisema kuwa teknolojia mpya pia itakuwa na manufaa kwa wachimbaji wadogo kwa kuwa mbali ya kulinda afya zao lakini pia itasaidia kuwaongezea kipato kwani wataongeza uzalishaji wa dhahabu.

# SUA yapewa bilioni 74/- kuboresha elimu, ajira

**Na Christina Haule,** MOROGORO

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimepokea Sh. bilioni 73.6 kwa ajili ya kuboresha elimu na kurahisisha upatikanaji wa ajira na kukuza uchumi kwa wahitimu.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala wa SUA, Prof. Amandus Muhairwa, alibainisha hayo wakati wa uzinduzi wa kamati ya ushauri wa viwanda na kuzungumza na watekelezaji wa mradi wa elimu na mageuzi ya kiuchumi (HEET) uliofanyika mjini hapa.

Prof. Muhairwa ambaye ni Mratibu wa Mradi wa HEET, alisema kupitia mradi huo, SUA imepokea fedha hizo ambazo kati yake, Sh. bilioni 55.2 zitatumika kutekeleza mambo mbalimbali ya SUA mkoani Morogoro na Sh. bilioni 18.4 zitatumika katika Kampasi ya SUA iliyopo nyanda za juu kusini.

Alisema kupitia mradi huo wanatarajia kufanya ujenzi wa majengo mapya, ukarabati na ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, uanzishaji na uboreshaji wa mitaala, kuanzisha na kuimarisha uwezo wa kiubunifu na utafiti wenye tija, kujenga uhusiano kiutendaji na sekta binafsi, kuimarisha matumizi ya TEHAMA, kujenga uwezo wa uzalishaji wa mapato ya ndani na kuwajengea uwezo wanataaluma na viongozi.

Prof. Muhurwa alisema katika kuanzisha mitaala mipya na kuhuisha mitaala, jumla ya mitaala 108 itahuishwa ili kuwezesha wahitimu kujiajiri na kuajiri, kuongeza mbinu za ubunifu katika ufundishaji sambamba na kujenga uwezo wa watumishi kielimu.

Alibainisha kuwa mpaka sasa wanataaluma 41 wa shahada za umahiri na uzamivu wanaendelea na masomo katika vyuo mbalimbali nchini na nje ya nchi.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, alisema katika kuboresha elimu kwa vyuo vikuu nchini, serikali imetenga dola za kimarekani milioni 425 sawa na Sh. bilioni 972 za kitanzania lengo likiwa ni kuimarisha ajira na kukuza uchumi wa wahitimu wa vyuo vikuu nchini.

Alisema mradi huo unatekelezwa kupitia mkopo nafuu wa fedha kutoka Benki ya Dunia ambao unatekelezwa kwa miaka mitano kuanzia 2021 ukihusisha vyuo vikuu 14 vya umma, taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Elimu zinazoshughulika na elimu ya juu ikiwamo CPU na COSTECH na taasisi tano zilizo chini ya Wizara ya Fedha.

"Tukiboresha elimu yetu, tukawa na rasilimali watu iliyo bora. Hapo ndipo tunaweza tukafanya kweli mageuzi hayo ya kiuchumi kama jina la mradi linavyoelezea," alisema Prof. Mdoe.

Aliwaagiza kutumia taratibu zilizowekwa katika kutatua changamoto wanazokumbana nazo na zikiwashinda, wawasilishe katika ngazi husika ili kutatuliwa kwa haraka na kufikia malengo kamili ya mradi na kukamilika kwa wakati.

Mwakilishi wa Benki ya Dunia, Kaboko Mkalinga, aliwataka washauri wa mradi kujitoa katika utekelezaji wa mradi huo kutokana na uzoefu walionao na kuhakikisha wanatoa mchango wao kwa wananchi ili mradi huo ufanikiwe kwa kuzalishaji ajira nyingi nchini.

HABARI KITAIFA

# Samia asema serikali itashirikiana na AZAKI ukuaji wa uchumi EAC

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema serikali itaendelea kukuza ushirikiano na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa kutunga sera ambazo zitakuwa chachu ya ukuaji wa uchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Amesema mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), unaelekeza kuwapo kwa ushirikiano wa kikanda na maendeleo katika jumuiya, utazingatia watu na uendeshaji wa masoko ya kibiashara.

Rais Samia alieleza hayo jana katika hotuba yake, wakati akifungua kongamano la kwanza la Jumuiya ya Asasi za Kiraia ya Afrika Mashariki, unaoendelea jijini Arusha kwa siku tatu, iliyosomwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima.

"Serikali ya Tanzania inaamini kwamba kongamano hilo, litaandaa mikakati ya wazi ya ushirikishwaji ili kuhakikisha kuna kuwapo kwa ushiriki wa Azaki kama sauti ya wananchi katika ngazi ya kikanda.

"Tunaamini kwa dhati kwamba ushiriki wa watu kupitia Azaki ni muhimu katika kuhakikisha sera zinafanya kazi mashinani kwa kuwa tunatambua nafasi na umuhimu wa Asasi za Kiraia kufanya utafiti na mijadala ya mikutano ya hadhara kuhusu masuala muhimu yanayohusu wananchi," alisema.

Pia alisema eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika (AfCFTA) ni mpango maalum uliowekwa kurahisisha ushirikiano wa kiuchumi wa Afrika na biashara za ndani na kujenga uthabiti dhidi ya majanga ya kimataifa.

Alisema AfCFTA kuhusu wanawake na vijana imedhamiria kuwa ya mabadiliko kwa kuwa itachangia ukuaji wa maendeleo endelevu barani Afrika.

Rais wa Asasi za Kiraia za Afrika Mashariki, Daniel Lema, alisema lengo la kongamano hilo, ni kuzikutanisha pamoja asasi hizo kwa kuwa sehemu ya kiungo baina ya wananchi wa eneo hilo na vyombo vinavyosukuma shughuli za mtengemano ndani ya EAC.

Alisema itasaidia kupunguza na kuondoa kabisa pengo lililoko kati ya watu, asasi za kiraia, serikali na vyombo vinavyofanya kazi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.



Mkurugenzi wa Bonde la Mto Pangani, Segule Segule (katikati), akikagua mtaro wa maji katika Mji mdogo wa Mirerani juzi, uliochimbwa na bonde hilo kunusuru zaidi ya watu 5,000 wa kata tano za Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha na Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, waliokuwa wanakumbwa na mafuriko. Kushoto ni Mhandisi wa Mazingira, Arafa Maggid na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Tanesco, Justin Abraham. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kesi 96 utelekezaji wa familia ziripotiwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

HALMASHAURI ya Mji wa Babati mkoani Manyara, imepokea kesi 96 za kutelekeza familia, huku watoto wachanga na wanawake wakiwa waathirika wakuu.

Idadi hiyo imeripotiwa katika robo ya mwaka 2022/23, ambapo pia wanaodaiwa kushiriki vitendo hivyo ni wenye uwezo wa kifedha.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri hiyo, Aghatha Patrice, alisema hayo wakati wa mahojiano maalumu na Nipashe huku akibainisha kuwa kwa siku wanapokea malalamiko manne mpaka matano ya kutelekezwa kwa familia.

"Kwa wiki tunapokea malalamiko ya kutelekeza familia tisa mpaka 10, na kwa mwezi tunapokea malalamiko 20 ila kwa robo mwaka tunakuwa na malalamiko 96,"alisema Patrice.

Aidha, alisema kesi nyingi wanatafuta mwafaka na zingine zinafikishwa mahakamani.

Ofisa huyo, alisema asilimia kubwa ya watu wanaotelekeza watoto ni wanaume na wachache ni wanawake ambapo alieleza kuwa watoto wengi ambao wanaotelekezwa ni wa miaka miwili mpaka mitano.

Alitaja madhara ambayo wanapata watoto kuwa ni kubakwa, kulawitiwa na kupata maradhi ya utapiamlo.

Naye Mkuu wa Dawati la Jinsia la Polisi Wilaya ya Babati, Daud Danyace, alisema suala la utelekezaji wa familia siyo kwa watu wa hali ya chini, ila na wenye uwezo wa kifedha wanatelekeza familia.

Mwenyekiti wa Shujaa wa Maendeleo Mkoa wa Manyara (SMAUJATA), Lightness Maina, alisema ili kutokomeza ukatili wa kutelekeza familia ni vizuri ziwepo nyumba za kuwahifadhi watoto ili wazazi wakipatana ndio watoto warudishwe nyumbani.

# Vifaa tiba mil. 88/- vyanaswa vikiingizwa kwa njia ya magendo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imenasa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 88 vilivyokuwa vikiingizwa nchini kwa njia ya magendo.

Kaimu Meneja wa TMDA Kanda ya Kaskazini, Proches Patrick, alisema jana kuwa mamlaka hiyo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Arusha, walifanya ufuatiliaji na kukamata dawa na vifaa tiba hivyo mpakani.

Alisema baada ya kukamatwa kwa dawa hizo, watazifanyia uchunguzi ili kubaini kama zina ubora unaotakiwa na taratibu zingine zianze kufuatwa.

Pia mamlaka hiyo imeweka wakaguzi wake katika vituo vyote vya forodha vilivyoko katika kanda hiyo ili kufanya ukaguzi na uchunguzi wa kimaabara kabla bidhaa hizo hazijaingizwa nchini.

Aidha alisema kuwa katika dawa na vifaa tiba hivyo, zinagharimu Sh.milioni 88 kati ya hizo Sh. milioni 86 kwenye dawa na vifaa tiba Sh. 2,000,000.

"Biashara za magendo sasa hivi zinazidi kupungua siku hadi siku kutokana na timu za operesheni zinazofanya kazi vizuri katika maeneo mbalimbali.

"Dawa hizo na vifaa tiba vilikamatwa na TRA vikiingia nchini kwa njia za magendo bila kupata vibali vinavyotakiwa na kukamatwa kwake ni kutokana na kuwa serikali iko makini kwenye kuhakikisha hakuna yeyote anayeingia kimagendo nchini, kwani kwa kufanya hivyo ni ukiukwaji mkubwa wa sheria za nchi yetu,"alisema.

Pia alisema kwa mfanyabiashara yeyote anayetakiwa kuingiza dawa nchini ni lazima bidhaa yake isajiliwe na iwe salama kwa mtumiaji, kinyume na hapo hatua kali za kisheria lazima zichukuliwe dhidi yao.


Alitoa onyo kwa wale wote wanaoingiza au kutengeneza bidhaa za dawa na vifaa tiba, bila kuzingatia matakwa ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219 kuwa waache mara moja na TMDA haitamwonea huruma yeyote atakayebainika kukiuka matakwa ya sheria hiyo.

Alitoa wito kwa wananchi kutoa taarifa za mtu yeyote anayeuza, kuingiza au kutengeneza dawa, vifaa tiba au vitenganishi bila kuzingatia Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba ili kuzifanyia kazi kwa na kuwachukulia hatua kali wahusika.

Meneja wa TRA Mkoa wa Arusha, Eva Raphael, alisema wafanyabiashara wanavyopitisha bidhaa hizo kwa njia za magendo, kuna tozo za TRA wanazotakiwa kulipia na za taasisi zingine wanazikwepa na hivyo kuikosesha serikali mapato.

Alisema baada ya kukabidhi bidhaa hizo kwa TMDA na kuzifanyia ukaguzi na kuangalia kama zinafaa kwa matumizi, zitachukuliwa na serikali kwa ajili ya hatua zingine zinazofuata.

"Ninawaomba tu jamani wale wote wanaofanya biashara hizo za magendo kuacha mara moja, kwani serikali ipo makini ni vizuri kila mmoja afanye kazi yake, kwa kufuata sheria na taratibu za nchi, ili kuepukana na hasara anayoweza kupata kama hizi za kutaifishwa bidhaa zote," alisema.



## Serikali na KCB kuwezesha vijana

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imeahidi kuendeleza ushirikiano na Benki ya KCB kupitia mradi wake wa tujiajiri katika kuwawezesha vijana katika masomo ya ujuzi na kujiajiri kwa kuwatengenezea mazingira mazuri ya kuzitumia fani mbalimbali walizojifunza ili kupunguza wimbi la vijana wasio na ajira mitaani.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, alisema hayo jana alipomwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, katika hitimisho la mafunzo kwa wanafunzi 295 kutoka Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) mkoani Mwanza. Wanafunzi hao walisomeshwa kupitia mradi wa tujiajiri chini ya ufadhili wa KCB na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (CIZ).

Alisema serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya utendaji kazi vyuoni pamoja na majengo ya kujifunzia, vifaa na vyumba vya madarasa ili kuhakikisha vijana wanasoma kwa vitendo na kuondoka vyuoni wakiwa na ujuzi utakaowawezesha kujiajiri katika fani zao.

"Mmeonyesha mfano mzuri wa kuwafikia vijana kwa kuwapa elimu pamoja na vitendea kazi watakavyovitumia huko waendako. Hatua hii itasaidia kupunguza wimbi la vijana wasio na ajira mtaani na sisi kama serikali tutaendelea kuwa pamoja na nyinyi kuwezesha hatua hizo za kimaendeleo," alisema Masala.

Naye Mkuu wa Uhusiano wa KCB, Christine Manyenye, akizungumza wakati wa kukabidhi vitendea kazi kwa wahitimu hao, alisema katika mkoa wa Mwanza tayari vijana 625 wenye umri wa miaka 18-35 kuanzia mwaka 2016.

Kadhalika alisema kupitia mradi huo, vijana 315 kutoka mikoa tofauti tofauti wamepata ajira baada ya kuhitimu mafunzo ya ujasiriamali yaliofadhiliwa huku wengine wakijiari katika shughuli za kiufundi walizosomea huku akiwataka vijana hao kuzitumia vyema taaluma zao kujikwamua kiuchumi.

"Kwa mwaka huu tumetoa wahitimu 295 ambao pia wamepatiwa vifaa vya kuwasaidia katika shughuli zao za kiufundi na mradi umegharimu zaidi ya Sh.milioni 94," alieleza.

Baadhi ya wahitimu wa mafunzo ya ujasiriamali waliiomba serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji katika chuo cha ufundi VETA Mkoa wa Mwanza ili kuwaimarisha vijana katika taaluma zao.

# Uchakavu mitambo TANICA washusha uzalishaji

**Na Titus Mwombeki,** BUKOBA

KIWANGO cha uzalishaji katika kiwanda cha Kahawa cha TANICA kilichoko katika Halmashauri ya Bukoba mkoani Kagera, umeshuka kutoka tani 500 hadi 300 kutokana na uchakavu wa mitambo.

Kutokana na uchakavu huo, uzalishaji katika kiwanda hicho huku kikihitaji zaidi ya Sh. bilioni 50 kwa ajili ya marekebisho.

Hayo yalibainishwa juzi kiwandani hapo na Meneja Mkuu wa TANICA, Mhandisi Rodness Milton, ambaye aliiomba serikali kutoa msaada katika kiwanda hicho ili kuinua shughuli za uzalishaji na kukidhi mahitaji ya soko la kimataifa.

Alisema fedha hizo zinahitajika kwa ajili ya kurekebisha miundombinu na kununua mitambo ya kisasa ili kuboresha shughuli za uzalishaji.

"Uzalishaji wa kiwanda hiki kwa mwaka zilikuwa tani 500 lakini kwa sasa umeshuka, hivyo kusababisha kushindwa kuingia katika ushindani na viwanda vingine. Tunaomba serikali kusaidiana na wanahisa katika kukinusuru kiwanda hiki hasa upatikanaji wa fedha zinazohitajika.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alisema serikali itakuwa bega kwa bega katika kusimamia ujenzi wa kiwanda hicho ili kuniwezesha kuwa na uzalishaji wenye tija na kutengeneza uchumi imara wa mkoa wa Kagera.

Chalamila aliongeza kuwa kupitia ombi la kujengwa kwa kiwanda kipya, kutasababisha hata wakulima ambao ndio wanazalisha wa malighafi za kiwanda hicho kuboresha zao hilo likiwa shambani.

Naye Katibu Tawala Msaidizi (Uchumi na Uzalishaji) wa Mkoa wa Kagera, Isaya Tendega, alisema mahitaji ya kiwanda kipya ni makubwa ili kufikia wastani wa kuzalisha kahawa na kulifikia soko.




Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Dominicus Lusajo (wa tatu kulia), akizungumza wakati wa mkutano wa kukaribisha wajumbe wa kamati ya maendeleo ya mkoa huo jana, ambao wako katika ziara ya mafunzo ya kutembelea miradi iliyotekelezwa kwa fedha za huduma kwa jamii (CSR), zilizotolewa na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu katika mikoa ya Shinyanga na Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara Sirari walia na mrundikano wa taka sokoni

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAFANYABIASHARA na baadhi ya wananchi katika mji wa Sirari, mkoani Mara wako hatarini kuugua magonjwa mbalimbali kutokana na soko na kituo cha magari mjini hapo kuwa na mrundikano wa taka.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao walisema mrundikano wa taka hizo katika soko na kituo cha magari, umekuwa ukiwatia hofu hususani katika kipindi hiki cha mvua kwa kuwa zinaweza kusababisha magonjwa ya mripuko kwa wafanyabiashara hao zaidi ya 300.

"Jalala hili limekuwapo hapa kwa muda mrefu sasa na tumezungumza mara nyingi kwa viongozi mbalimbali wa serikali lakini hatupati suluhu ilihali awali viongozi wetu, wakiwamo mbunge na diwani, walishiriki kuondoa jalala hili lakini limerudi tena na hakuna anayejali," alisema Marwa Mwita.

Bhoke Mwita ambaye ni mfanyabiashara katika soko hilo, alisema jalala hilo limekuwa likitoa harufu kali na kutiririsha maji kuelekea katika maeneo wanayofanyia biashara na kwenye makazi ya watu yaliyo jirani na soko hilo. Alisema hali inayohatarisha afya zao pamoja na wateja wao.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti katika soko na stendi hiyo mapema wiki hii, baadhi ya wafanyabiashara na wananchi waliojitambulisha kwa majina ya Mangera Chacha, Mwita Sasi, Elizabeth John, Matiko Lameck, Wesiko Nyamhanga na Gimase Mwita walisema: "Sisi wafanyabiashara tulioko ndani, nje ya soko na walioko nje stendi ya magari na wakazi wa mji huu wa Sirari tunapata wakati mgumu wa kufanya biashara zetu.

"Hii ni kutokana na rundo la uchafu uliokithiri na kutoa harufu kali na maji yanayotiririka kuelekea kwenye nyumba za makazi ya watu. Hali hii inatishia afya zetu kwa kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na kuharisha."

Pia alisema uchafu huo uloambatana, haujazolewa kutoka eneo hilo kwa kipindi cha zaidi ya mwezi mmoja, hivyo kuiomba serikali kufuatilia na kudhibiti kadhia hiyo inayohatarisha afya za wananchi, wafanyabiashara na wateja.

Amos Sagara, Diwani wa Sirari, alithibitisha uwapo wa rundo la taka hizo na stendi ya magari na kusema tayari amewasilisha kilio cha wananchi katika uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ili kuondoa haraka taka hizo kabla hazijaleta madhara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Solomon Shati, alisema tayari wameweka katika mpango wa kuondoa taka hizo na zinatarajiwa kuondolewa muda si mrefu.



Ukurasa 12

Reli ya kisasa SGR na ukaribisho wa maisha ya kisasa mapya kwa wakazi Kanda ya Ziwa



Ukurasa 13

Hili la vyeti vya udereva kwa kweli, halijakaa sawa



Ukurasa 14

Uwanja wa Ndege Moshi, miaka 59 ukisuasua, lakini ni nyeti kiuchumi

BUFE

IJUMAA MEI 5, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI

# Dondoo Rais Samia zilivyowakuna wafanyakazi kwenye Mei Mosi yao

**Na Sabato Kasika**

ILIKUWA simulizi ya namna yake, maadhimisho ya Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani Mwaka 2023, yalipambwa na kaulimbiu 'mishahara bora, ajira za staha ni nguzo kwa maendeleo ya wafanyakazi, wakati ni sasa'.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akawa mgeni rasmi katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro, kulikosheheni hadhira iliyooongozwa na viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), nyuma yao kuna umma wa wafanyakazi na wananchi kwa jumla, wakiguswa na kauli mbiu 'uadilifu na weledi kazini, ni chumbuko la maisha bora kwa wafanyakazi'.

Kikuu kwanza kuvutia hadhira hiyo, ni ahadi ya mwaka jana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye akawaahidi wafanyakazi mwaka jana katika kile anatumia msamiati 'jambo letu' kwa maana ya maslahi, kwamba pande mbili zingekutana kuyajadili hayo.

Katika hotuba yake Rais Dk. Samia siku nne zilizopita, zilijaa mambo ya kuwatia moyo wafanyakazi, hata 'kuwakuna' katika namna ilivyojikita katika mambo makuu kadhaa, yanayogukia katika sura kuu mbili, yaani utekelezaji wa serikali kwa maslahi ya wafanyakazi, pili ahadi kwao.

Rais Dk. Samia akaweka bayana kuhusu utekelezaji wa madai ya malimbikizo ya wafanyakazi, akisema jumla yake yalikuwa 14,516 na kwamba tayari serikali imeshafanyia kazi madai 13, 523, huku akifafanua kwamba yamebaki machache.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwasalimia wafanyakazi katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro katika siku ya Mei Mosi wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

Hapo akafafanua nafasi ya waajiri kutowasilisha michango ya wafanyakazi wao katika mifuko ya hifadhi ya jamii, rais akisema ameshamwagiza waziri mwenye dhamana ya ajira pamoja na waziri mkuu, kufanya mkutano na waajiri ili wafanyakazi walipwe stahiki zao katika namna inayohitajika.

Mnamo Mei mwaka jana, Rais Samia aliridhia mapendekezo ya kuongeza mishahara, ikiwamo kima cha chini kwa watumishi wa umma asilimia 23.3 na fedha kiasi cha shilingi trilioni 1.59 ikatumika kuongeza hitaji hilo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jambo ambalo wiki hii akalianika kwamba limeshatekelezwa kwa wafanyakazi hao wenye mishahara ya chini kwa asilimia 23 iliyopangwa katika bajeti ya sasa.

Eneo lingine la maslahi kwa wafanyakazi, Rais akasema Baraza la Kazi na Uchumi nchini limeshaelekezwa kusikiliza changamoto za mfumo wa fidia kwa wafanyakazi, ili iweze kutoa huduma, pia kuunda Kamati za Usalama Sehemu za Kazi, inayowajumuisha waajiri na wafanyakazi wenyewe.

Rais anafafanua kwamba, unahusu kuwaongezea watumishi vitendea kazi katika kitengo cha Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), ikiwa na maana ya kuendelea kuongeza wafanyakazi mahali hapo, pia magari ili kazi zake zifanyike kwa ufanisi.

**NYONGEZA KILA MWAKA**

Penye msamiati wa maslahi 'jambo letu' ambao Rais Dk. Samia aliutamka mwaka jana, sasa anataja mbinu mpya iliyowahi kuwapo zama zilizopita katika suala la nyongeza ya mshahara, wakati wa sikukuu ya mwaka huu mjini Morogoro.

Rais akafafanua staili ya nyongeza kufanyika kwa ukimya, hadi sasa namna ya utekelezaji wake unaendelea kufanyiwa kazi, rais akisema itaendana na kulipa malimbikizo ya madai katika bajeti ya mwaka wa fedha ujao.

Anafafanua kuwa, hatua hizo sasa itafanyika kwa ukimya, ikilenga kuwabana wafanyabiashara wanaovizia matangazo ya mishahara mipya, kwa kupandisha bei za bidhaa zao sokoni, Rais Dk. Samia akiitafsiri inawaumiza watu wenye kipato cha chini.

'Wafanyakazi mambo ni moto...mambo ni fire,' akasikika Rais Dk. Samia wakati akitangaza kurejesha nyongeza ya mishahara ya kila mwaka kwa wafanyakazi wa umma, ikiwa ni miaka saba tangu kuondolewa mwaka 2016.

INAENDELEA UK.14

BIASHARA

# Reli ya kisasa SGR na ukaribisho wa maisha ya kisasa mapya kwa wakazi Kanda ya Ziwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATIKA mikoa mitano iliyopo katika Kanda Ziwa kumekuwa na fursa nyingi za kiuchumi, ambayo pia inagusa, kutoka Dar es Salaam, kwenda mikoa hiyo, hali kadhalika zinazoenda nchi za kigeni, katika mataifa jirani ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC) na Rwanda.

Hao wavukao mipaka, hutumia muda mrefu kuhesabu siku nyingi, inaathiri biashara katika maeneo husika, ikiwamo kuuzwa kwa bei ya juu.

Sasa, tukio la kazi ya ujenzi wa reli ya kisasa kilomita 165, kutoka mkoa wa Tabora hadi Mji Mdogo wa Isaka, ni ujenzi wa kipande kinasaidia katika kukuza uchumi wa mikoa hiyo kupitia rasilimali zilizopo.

Ikiangaliwa katika mkoa wa Tabora, kuna fursa kubwa kutoka zao la tumbaku, hali ambayo reli inapokamilika, inaleta neema ya kujengwa viwanda vingi katika mkoa huo, kwani wawekezaji watakuja kwa wingi kwa kuvutiwa na mazingira ya miundombinu.

Vilevile inatajwa, kwa kutumia reli hiyo, pia inakuwa fursa kubwa katika kukuza baadhi ya mji iliyopo pembezoni mwa reli hiyo, pale vinapojengwa vituo vya kisasa kwa ajili ya abiria na mizigo hasa katika miji ya Isaka, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga na mkoa wa Tabora.

Ni matarajio kwamba, reli itapunguza mwendo wa muda mrefu wa magari ya mizigo, hasa yale yanayoenda katika nchi za jirani, kwani yapo yanayotumia wastani wa siku saba hadi 30 katika safari za kwenda na kurudi, vyote vinatarajiwa baada ya reli kukamilika kuingia katika mabadiliko makubwa katika eneo hilo la usafirishaji.



Sehemu ya barabara ya Isaka –Ushirombo, wilayani Kahama, ambako magari makubwa ya mizigo, yakiwamo yaendayo nchi jirani zikitoka na kwenda bandarini Dar es Salaam, zinapita sasa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### MKURUGENZI TRC

Mhandisi Masanja Kadogosa, Mkurugenzi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), anasema vipande vyote vinne vya ujenzi wa reli hiyo ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi jijini Mwanza, hadi zaidi ya mwezi mmoja uliopita, makandarasi na ujenzi wake wanaendelea na wananchi wamepata fursa ya kupata ajira za muda, huku taarifa ya hivi karibuni ya kiserikali muda mfupi uliopita ni vichwa vya treni vimeingizwa nchini kwa majaribio.

> **Ni mradi unaotarajiwa kuwa fursa katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na serikali itakipanua Chuo cha Reli kilichopo mkoani Tabora, hata kikatoa shahada ya ngazi ya juu na tayari kimeshatoa ajira kwa watu 20, 000.**

Anasema, ujenzi wa reli hiyo ulianza tangu mwaka 2017 na una urefu wa kilomita 1,596, ukitarajiwa kuleta mafanikio makubwa katika mikoa hiyo na serikali ikiendelea na ununuzi wa mabehewa 89 kwa ajili ya kubeba abiria na mizigo.

Mhandisi Kadogosa anasema, mradi wa Tabora hadi Isaka unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi trilioni 2.6, ukichukua miezi 42 hadi kukamilika kwake mwaka 2026 na usanifu na utunzaji wa mazingira utazingatiwa.

"Ni mradi unaotarajiwa kuwa fursa katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na serikali itakipanua Chuo cha Reli kilichopo mkoani Tabora, hata kikatoa shahada ya ngazi ya juu na tayari kimeshatoa ajira kwa watu 20, 000," anasema Mhandisi Kadogosa.

### WAKAZI WA ISAKA

Juma Bundala, ni mkazi wa Mji Mdogo wa Isaka, ambako reli hiyo ya kisasa itapita, hivi karibuni akiambia Nipashe kuwa wakati umefika wa mkandarasi anayejenga reli hiyo kuona jinsi atawapa kipaumbele katika kuwapa kazi wananchi na hasa vijana wa eneo, ambao watakuwa na sifa.



Ujenzi wa reli ya kisasa, maarufu SGR ukiendelea.

Anasema, kumekuwa na tabia ya wakandarasi kuajiri watumishi kutoka nje ya eneo la mradi hali ambayo imekuwa ikileta malalamiko makubwa kwa wenyeji walipo katika mradi husika na kushindwa kunufaika kwa kupata kazi za muda mfupi.

Naye Nyamizi Masanja, anasema mkandarasi huyo ambaye ni kampuni ya Yap Markez, haina budi kuangalia ajira kwa upande wa wanawake, ili nao waweze kujipatia ajira na kuweza kuendesha maisha yao kama walivyo wanaume ikiwemo za usambazaji wa chakula kwa vibarua.

### WAKUU MIKOA KANDA

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yahaya Nawanda, anasema kukamilika ujenzi wa reli ya kisasa, kutasaidia kuleta maendeleo makubwa kwa wananchi wa mkoa wa Shinyanga na kuwataka kuchangamkia fursa zilizopo katika mradi huo, ili kujiingizia kipato maradufu.

Anataja kazi zinazoweza kufanywa na wananchi wa maeneo mradi unapopita, wapewe ili waweze kukuza uchumi wao, hali ambayo itawasaidia kuwatoa kwenye wimbi la umasikini katika familia zao na kupunguza wimbi la vijana wa mitaani wasiokuwa na ajira na wizi wa mafuta katika mradi.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Buriani, anasema reli hiyo itasaidia kuinuka kiuchumi wa mkoa wake, kwa wawekezaji kuiunga nao kiuchumi, kwani kwa sasa umekuwa hanuna viwanda na kusababisha malighafi yote kusafirishwa kwenda mikoa mingine yenye viwanda.

"Hakuna sababu kwa wawekezaji kutowekeza katika mkoa wa Tabora kwa kipindi hicho (reli ikikamilika), tunaweza kuwekeza katika mambo mbalimbali kama ujenzi wa Kiwanda cha Saruji kwa kuwa mali ghafi nyingi ya bidhaa hiyo inapatikana katika Mkoa huu," anasema Dk. Buriani.

Aidha, anaeleza kukamilika kwa reli hiyo, pia utafungua milango katika maeneo hasa ya pembezoni yaliokuwa hayana viwanda kupata wawekezaji, kwakuwa usafiri wa uhakika utakuwapo na bidhaa zitafika kwa wakati sokoni na viwandani.

### M/KITI KAMATI BUNGE

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Miundombinu, Moshi Kakoso, anakasema kampuni ya ujenzi ya Yap Markez, mpaka Februari meaka huu, ilikuwa hijalipaa wakandarasi wadogo wa mradi huo kiasi cha Sh.Bilioni 12 na akawataka kufanya malipo, kuondoa migogoro, ili mradi utakapokamilika kusiwe na madai yoyote.

Waziri wa Ujenzi na Miundombinu Makame Mbarawa, anakasema serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuwaletea wananchi miundominu mizuri katika kipindi hicho na akiwataka kuchangamkia fursa pale miradi mikubwa ya kimkakati inapoanzisha na kujiingizia kupato.

### MAKAMU WA RAIS

Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, anasema, mradi wa Reli ya kisasa ni wa mfano barani Afrika na kutokana na hali hiyo serikali imeamua kuwekeza sekta ya usafirishaji ili kuhakikisha wananchi wake hawapati shida na bidhaa zinafika sokoni kwa wakati.

Anasema, ujenzi wake utasadia katika kuweka mazingira mazuri ya biashara na kuliweka Taifa katika ushindani wa kibiashara huku akisisitiza ni lazima usimamiwe ili uweze kumalizika kwa wakati na kuanza kuwanufaisha wananchi pamoja na wafanyabiashara.

Aidha Dk. Mpango anasema, serkali imewekeza uwekezaji katika reli na Bandari, katika ujenzi wa reli hiyo jumla ya ajira 20,000 zimepatikana zenye thamani ya Sh.bilioni 237.6 ambazo zitatumika kulipa mishahara, shilingi trilioni 1.9 zimetumika katika zabuni huku serikali ikikusanya Sh.bilioni 949 kama kodi.

Hata hivyo Dk. Mpango anasema sehemu kubwa ya fedha za mradi huo ni mkopo na hakuna ubaya wowote wa kukopa nakwamba serikali haitaacha kukopa na uwezo wa urejeshaji upo na kuwataka viongozi na wasimamizi kusimamia fedha hizo vizuri ili mradi ukamilike kwa wakati na kutoa huduma zilizolengwa kwa wananchi na malengo ya kitaifa.

## Dondoo za Rais Samia zilivyowakuna wafanyakazi kwenye Mei Mosi yao

INATOKA UK.11

### AHADI NYINGINE

Rais Dk. Samia anafafanua ahadi kuwa serikali itajitahidi kuwekeza na kuvutia uwekezaji nchini, kujenga uchumi, ili kutengeneza nafasi zaidi za ajira kitaifa kwa maslahi ya wafanyakazi wakiwa ni kipaumbele.

Hapo anatoa rai kwa vyama vya wafanyakazi viendelee kushikamana, huku serikali kwa upande wake ikifanya jitihada za kuhakikisha inaboresha maslahi yao, ikiwa ni sehemu ya umma kuendelea kuwa na maisha bora.

"Serikali itajitahidi kuwekeza na kuvutia uwekezaji, kujenga uchumi ili kutengeneza nafasi zaidi za kazi, kujenga uchumi ili maslahi yanayodaiwa na wafanyakazi yaweze kupatikana," anasema.

Lingine ni pale Rais Dk. Samia anapokumbusha kwa msisitizo kuwa, suala la uadilifu na weledi kazini ni muhimu kwa kila mfanyakazi, kwa kuwa ndio chimbuko la maisha bora kwao mahali walipo.

Kuhusu nafasi ya pekee kwa taaluma ya ualimu, ambayo kimsingi ina kundi kubwa la watumishi nchini wanaangukia ofisini kwake, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), huku kitaaluma wakiwa wanaunda nguzo ya uelewa na utaaluma kitaifa na kimataifa, Dk. Samia anagusia dai la haki zao lililoibuka bungeni hivi karibuni, kuhusu kuwapo posho za kufundishia.

Hapo rais akaahidi kulifanyia kazi kama walivyoomba, jibu hilo akiunganisha na dai linalohusu matumizi ya vishikwambi (tablets), ambazo wamepewa walimu kutekeleza majukumu yao, baada ya kutumika kwenye Sensa ya Watu na Makazi mwaka jana.

Siku chache zilizopita, Mbunge wa Kilwa Kusini mkoani Lindi, Ally Kasinge, akaibua hoja bungeni, jijini Dodoma kwamba elimu inaendelea kudorora kutokana na kuondolewa kwa posho ya kufundishia kwa walimu, akidai kwa sasa walimu wengi wamekata tamaa na kukosa ari ya kufundisha kwa madai kwamba kuondolewa kwa posho hiyo kunachangia hayo yote.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Hili la vyeti vya udereva kwa kweli, halijakaa sawa







**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

WIKI iliyopita nilikuwa mmoja wa wanahabari waliotembelea Hospitali ya Benjamin Mkapa, iliyoko katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), katika ziara iliyoratibiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Tulitembelea hospitali hiyo, kwa lengo la kujionea ni kwa kiasi gani NHIF imewekeza katika suala zima la matibabu kwa Watanzania na hususan wanachama wake, ambao hata hivyo si wengi sana nchini.

Jambo kuu lililotuvutia watalii sisi, ni utaratibu wa wagonjwa walio wanachama kujisajili na kupata matibabu. Kuna ile dhana ya kutotumia karatasi asilani kama ilivyokuwa awali.

Tunakumbuka jinsi huko nyuma ilivyokuwa lazima kuandikisha cheti ili kumwona daktari na hata kufungua jalada lako la kumbukumbu za matibabu, ambayo mgonjwa alifika na kadi na kupewa jalada na kuzunguka nalo.

Kwa wagonjwa wa mara kwa mara, ni dhahiri jalada lilijaa na hata kuchakaa kutokana na wingi wa karatasi na ile zunguka zunguka nalo naweka toa kwenye makabati ya hospitali husika.

Kwa hospitali ya Benjamin Mkapa, mambo yamebadilika kabisa, ambayo sasa mgonjwa anatambuliwa kwa sura na alama za vidole na mawasiliano kuanzia hapo kidigitali. Hakuna karatasi kabisa.

Nimetoa bashraf hii, hasa kutokana na kinachotaka kufanyika nchini, kuhusu madereva wetu barabarani, eti kulazimika sasa kutembea na si tu leseni zao, bali pia vyeti vya udereva kutoka vyuo walivyosomea.

Tena kuna tangazo kuwa ukingoio mwa mwezi huu ndio mwisho wa kuhakikisha vyeti hivyo vipo na baada ya hapo utaanzishwa ukaguzi wa Jeshi la Polisi wa Usalama Barabarani, dhidi ya madereva watakaokuwa hawana vyeti.

Inashangaza kuwa wakati huu ambao watu wanatambulika kwa kado za uraia za NIDA, sasa tunataka kurejea kwenye analogi, kwa kutembea na vyeti. Kidogo kidogo baada ya hili, bila shaka tujiandae kutembea na vyeti vya kuzaliwa na vya ndoa.

Hivi kweli serikali haina uwezo wa kujua leseni gani ni bandia na ipi ni halali, mpaka kufikia kulazimisha madereva kutembea na vyeti? Inajulikana madereva leseni zinapomaliza muda hutakiwa kuzihuisha. Inakuwaje leo watiliwe shaka?

Nadhani polisi wanatakiwa kutafakari hatua hili, kwa kufanya ukaguzi wa kawaida tu wa leseni na watakapobaini dereva na leseni bandia basi waanzie hapo kwa kumchukulia hatua.

Dereva kajifunza au dereva miaka ya sabini, leo unamwambia atafute cheti chake atembee nacho barabarani, atakitoa wapi? Kwanza wakati huo nchi ilikuwa na vyuo vingapi vya udereva?

Wengi wa madereva walijifunzia majumbani kwa ndugu zao, baadhi walijifunzia kazini, mathalan jeshini ambako unaweza kujua udereva bila hata kutarajia, leo mstaafu anaendesha gari lake barabarani, asimamishwe na kuombwa cheti kweli!

Hatukatai kwamba ajali za barabara nini nyingi, lakini sidhani kama zinasababishwa na leseni, kwani kuna mambo mengi, hata wenye leseni za vyeti vya vyuo vikuu vya udereva, kama vipo wanaweza kusababisha ajali kwa sababu yoyote.

Lakini, bado gari linaloendeshwa na dereva mwenye shahada ya udereva, kama ipo,linaweza kusababisha ajali kutokana na ubovu wa muda mrefu au hata wa ghafla.

Miundombinu mibovu ya barabara nayo ina mchango mkubwa katika kusababisha ajali barabarani. Hivyo haitoshi kutazama tu leseni, kwamba ndicho kiini cha kusababisha ajali hizo.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), bila shaka ina kanzi data ya leseni za madereva wote nchini, hali kadhalika Jeshi la Polisi ambalo ndilo lenye mchango mkubwa sana katika kuthibitisha uhalali wa mtu kupewa leseni.

Tusijiegemeze kwenye vyeti, tukiamini kwamba ndiko kuliko na ujuzi au umahiri wa kufanya jambo, kwamba kama dereva hakupitia chuo cha udereva, basi hawezi kuelekezwa hata huko barabarani kwa kupewa elimu na kuwa bora.

Tutajikuta tunapanua wigo wa rushwa kwa baadhi ya askari wetu wasio waaminifu, ambao wengine tumekuwa tukiwashuhudia mchana kweupe wakiomba na kupokea chiochote.

Tumekuwa kila mwaka kwenye Wiki ya Nenda kwa Usalama, baadhi ya askari wasio waaminifu wakiigeuza kama wiki ya kivuno kwa kuuza stika, tukiambiwa kwa bei kati ya Sh 5,000 na Sh 7,000 kutegemea ukubwa wa gari, bila hata kufanya ukaguzi. Hebu basi tulitazame hili kwa jicho la tatu.

Alamsiki!

BIASHARA

# Uwanja wa Ndege Moshi, miaka 59 ukisuasua, lakini ni nyeti kiuchumi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

NI ngumu kutenganisha maendeleo ya mkoa wa Kilimanjaro na Uwanja Mdogo wa Ndege wa Moshi toka mwaka 1954,"anasema mbunge wa jimbo la Moshi Mjini mkoani Kilimanjaro Priscus Tarimo.

Anasema uwanja huo, umekuwa msaada kwa watu wa mkoa wa Kilimanjaro, mikoa ya jirani na nchi jirani hasa katika sekta ya utalii, matibabu na biashara.

Uwanja huo mkongwe wenye takribani miaka 69 sasa, bado unakabiliwa na uchakavu wa miundombinu hasa barabara ya kutua na kuruka ndege zinazokidhi mahitaji ya uendeshaji kwa sasa,ukosefu wa jengo la abiria, uzio wa usalama kuzunguka eneo la kiwanja unaosababisha wananchi kukatiza kiholela kwenye maeneo ya kiwanja.

Pamoja na juhudi mbalimbali za ulinzi zinazofanyika ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa wananchi lakini bado hazijafanikiwa,hali hii imesababisha barabara ya kutua na kurukia ndege ya kiwango cha nyasi (grass runway 18/36) kufungwa na kukosekana kwa gari la zimamoto, ambalo ni muhimu katika shughuli za uendeshaji wa uwanja wakati wa dharura.

"Uwanja huu ni moja kati ya viwanja 59 ambavyo vinamilikiwa na mamlaka ya viwanja vya ndege Tanzania, ambacho ni kikongwe kilifunguliwa mwaka 1954 ambao upo Magharibi mwa mji wa Moshi takribani kilometa nne toka mjini kati,"anatoa historia na kuendelea:

"Kiwanja hiki kilianza kufanya kazi na Serikali ya Malkia Elizabeth. Kinaitwa Moshi Aerodrome & King George VI Playing Field. Kuanzia miaka ya 1999 kiliendeshwa chini ya idara ya serikali katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi wakati huo na kuanzia mwaka 1999 mwishoni, kiwanja kinaendeshwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA)," anaeleza mbunge

Anafafanua kwamba, miundombinu iliyopo kwenye kiwanja hicho kina ukubwa upatao hekta 296 zimeshapata miliki tangu mwaka 2006, kukiwapo barabara mbili za kutua na kuruka ndege, moja ya kiwango cha lami yenye urefu wa mita 1,268 na upana mita 30.

Tarimo anataja nyingine, ni ya nyasi yenye urefu wa mita 1480 na upana wa mita 30, kukiwapo barabara mbili za viungio (Taxi ways) pamoja na maegesho ya ndege (Apron) kwa kiwango cha lami.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, Uwanja wa Ndege Moshi una fursa kubwa za kibiashara katika nyanja za kitalii kwa kanda ya Kaskazini, ikiwamo kupanda Mlima Kilimanjaro na kutembelea vivutio vya asili.

"Mnada wa kahawa unafanyika katika Bodi ya Kahawa (TCB), wafanyabiashara kote duniani hushiriki na wapo baadhi yao walikuwa wakitumia uwanja huo katika kurahisisha muda wa watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro, wengi walitumia uwanja huo " anasema.

Anaendelea kufafanua kuwa, uwanja huo unatumika pia katika suala la uokoaji katika maeneo mbalimbali hasa miji ya Mlima Kilimanjaro pamoja na kusaidia uzimaji wa moto katika mlima huo, pia kuna usafirishaji wagonjwa mbalimbali wanaohitaji matibabu ya haraka kwenda kama Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) au nchi jirani, ikiwamo jijini Nairobi, Kenya.

Lingine analolitaja ni kutumika ndege zisizozidi uzito wa kilo 31,600, ambazo zinatoa huduma za zimamoto, kulingana na viwango vya Shirika la Kimataifa la Usalama wa Usafiri wa Anga (ICAO).

Vilevile, kunatajwa kuwapo karakana kwa ajili ya matengenezo ya ndege, huku asasi ya madaktari wanaosafiri nao wakitumia kiwanja hicho, kwa ushirikiano na Hospitali ya Rufani ya KCMC, ikiwachukua madaktari na wagonjwa kuwapeleka na kuwarudisha sehemu mbalimbali, kwa ajili ya huduma za kitabibu na kuna kampuni pia watu binafsi wanao hifadhi ndege zao mahali hapo.

Katika majukumu, Tarimo anafafanua kwamba kiwanja hicho kwa sasa inasimamia viwanja viwili vidogo (airstrips), ambavyo ni Kiwanja cha Same Kiwanja cha Ndege cha West Kilimanjaro.

Tarimo anasema, serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 12 kwa ajili ya ukarabati wa uwanja huo, ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba mwaka huu, utakaosaidia ukuzaji utalii na uchumi kwa ujumla.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), mkoa wa Kilimanjaro ambao ndio wasimamizi wa ukarabati huo wa uwanja, Mhandisi Motta Kyando, anasema malengo ya mradi huo ni kuboresha usafiri wa anga, kwa ajili ya kuinua Pato la Taifa kupitia sekta ya Utalii.

Anasema, kwa kuzingatia umuhimu wa viwanja vya ndege, ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi, utaleta matokeo chanya ya ongezeko na kukuza sekta ya utalii.

"Mkataba wa ukarabati wa kiwanja hicho ulisainiwa Septemba 30 mwaka jana na kuanza rasmi Novemba 18 mwaka jana, ambao unategemewa kukamilika Novemba 18 mwaka 2023. Kulingana na usanifu maboresho ya Kiwanja cha Ndege cha Moshi, yanahusisha kufanya ukarabati wa njia mbili za kutua na kuruka ndege pamoja na ujenzi wa maeneo ya usalama," anasema.

Mhandisi anafafanua: "Maboresho ya maegesho ya ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka uwanjani, kuweka uzio wa usalama katika kiwanja pamoja na kutengeneza barabara ya mzunguko ndani ya kiwanja na kujenga mitaro na karavati za kutolea maji."

### RC KILIMANJARO

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alipotembelea kiwanja hicho kushuhudia hali halisi, akamtaka mkurugenzi kuhakikisha wote waliovamia uwanja huo wanaondoka, ili kabla ya mkandarasi kukabidhi uwanja huo Novemba mwaka huu, awe ameshaweka uzio kuzunguka uwanja huo.

"Tumesikia hapa uwanja huu unatakiwa kuwekewa fensi, lakini changamoto ni baadhi ya wananchi ambao wamevamia katika eneo la uwanja na kujenga makazi sasa na kuagiza Mkurugenzi wa Manispaa, hakikisha watu hao wanaondoka mara moja ili kupisha shughuli za ukarabati zinazoendelea katika kiwanja hiki" anasema

Mkuu wa Mkoa anasema, uwanja huo wa ndege una muda mrefu, lakini ni sehemu muhimu kwa mkoa, hivyo anamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu, kuona umuhimu wa kuufanyia ukarabati uwanja huo.

Anasema, kukamilika kwa ukarabati huo kutachangia kuongezeka watalii wanaoenda kwenye Mlima Kilimanjaro wanaopitia mahali hapo.



Mbunge wa jimbo la Moshi Mjini, Priscus Tarimo, akipewa maelezo kuhusu Uwanja wa Ndege wa Moshi **PICHA: MARO MOSHA**



Picha ya Uwanja wa Ndege wa Moshi, kutoka angani. **PICHA: MTANDAO.**

> **"Kukamilika kwa ukarabati huo kutachangia kuongezeka watalii wanaoenda kwenye Mlima Kilimanjaro wanaopitia mahali hapo.**



# COSTECH yawataka wabunifu kuchangamkia fursa za ufadhili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imewataka wabunifu kutumia fursa zinazotolewa na serikali kuendeleza ubunifu wao ili utambuliwe na kuingia kwenye ushindani kitaifa na kimataifa.

Jijini hapa jana, Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alisema serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA) na Mfuko wa Ubunifu wa Maendeleo ya Watu (NDIF), wametoa fedha kwa ajili ya kusaidia kuendeleza kazi za ubunifu.

"Wabunifu ongezeni jitihada katika kazi za ubunifu mnazofanya. Serikali iko kwa ajili ya kuwasaidia ndio kila mwaka kumekuwa na mashindano na wiki ya ubunifu kwa ajili ya kuona kazi zenu," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa kuanzia mwaka 2018 hadi 2022, COSTECH imewatambua wabunifu 2,647 na kati ya hao 283 wamepatiwa msaada wa kitaalamu na wengine 178 wamepatiwa fedha ili kuendeleza ubunifu wao kwa ajili ya kutambulika kitaifa na kimataifa.

"Hizi zote ni jitihada za serikali kuhakikisha wabunifu wanapiga hatua katika kile wanachofanya ili kusonga mbele, hivyo wabunifu waje na kazi bora ili zitambuliwe," alisema.

Meneja wa Teknolojia wa COSTECH, Dk. Erasto Mlyuka, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau imetoa Sh. bilioni 4.2 kwa ajili ya kusaidia ubunifu na kuratibu vituo vya teknolojia vya kuendeleza kazi za wabunifu.

Dk. Mlyuka alisema kuanzia mwaka 2018 hadi 2022, Sh. milioni 200 zilitolewa kwa ajili ya kuendeleza uvumbuzi na Sh. bilioni 3.3 zilitolewa kwa wavumbuzi. Sh. milioni 740 zilitolewa kwa ajili ya programu za uvumbuzi zinazofanyiwa kazi.

# RC apiga marufuku shughuli za kibinadamu Msitu wa Sekenke

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amepiga marufuku shughuli za kibinadamu katika Hifadhi ya Msitu wa Sekenke wilayani Iramba mkoani Singida ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Serukamba alitangaza marufuku hiyo juzi alipokuwa anasikiliza kero za wananchi wa Kijiji cha Masagi, Kata ya Mtoa wilayani hapo baada ya wananchi kuwasilisha ombi kwa serikali iwaruhusu kuchunga mifugo ndani ya msitu huo.

Alisema kufanya shughuli za kibinadamu kwenye hifadhi za misitu zinasababisha ukame ambao umekuwa ukiathiri shughuli za uzalishaji kama vile kilimo.

Mkuu huyo aliwataka wananchi wenye mifugo kutenga maeneo ya malisho na kuanzisha kilimo cha nyasi kwa ajili ya kulisha mifugo yao.

"Wazee ninyi mmekuwa hapa, kote huko kulikuwa na misitu kwa sababu wazazi wetu waliilinda misitu. Haiwezekani sisi tuache kulinda misitu. Mlima Sekenke lazima tuulinde. Habari ya kuchunga, kukata kuni huko haipo! Umefika wakati mtu awe anatenga eneo la kufugia na ardhi ambayo utalima," alisema. Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alisema kuharibiwa kwa misitu katika Kata ya Mtoa na maeneo mengine kumesababisha kuharibu vyanzo vya maji na kutopata mvua ya kutosha, hali ambayo imeathiri uzalishaji kulinganisha na awali kulipokuwa na misitu mingi ambayo ilikuwa inavutia mvua.

Mwenda alisema Wilaya ya Iramba ndiyo ilikuwa eneo pekee lenye vyanzo vingi vya maji yakiwamo mabwawa na Ziwa Kitangiri, Doromoni, Mabwawa ya Urughu na Mayanzani lakini kwa sasa kutokana na uharibifu wa misitu vyanzo hivyo, vimeathirika na vingine kukauka.



Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli (kushoto) na Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe De Boer, wakitiliana saini jijini Dodoma jana mkataba wa makubaliano na serikali ya nchi hiyo, kusaidia teknolojia ya kidijitali kwa wasafirishaji wa mizigo ya mazao ya nje ya nchi.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wasichana wapewa nafasi kiwanda kipya vishikwambi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMPUNI ya TANZTECH Electonics Limited inatarajia kuanza uzalishaji wa vishikwambi mwezi huu nchini, huku asilimia 90 ya waajiriwa wake ni wasichana kutokana na kutopewa nafasi katika teknolojia.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Gurveer Hans, alisema jana jijini hapa kuwa hadi sasa vijana wazawa 50 wamepatiwa mafunzo ambao asilimia 90 wana umri chini ya miaka 25 na asilimia 90 ni wasichana.

"Katika sekta hii ya teknolojia, wasichana hawapati fursa ya ajira kwa kiwango kikubwa, hivyo tumeona kampuni yetu iwaajiri wasichana na ndani ya miezi miwili tukianza uzalishaji tutaongeza idadi ya vijana kufikia 80 hadi 250," alisema.

Aliongeza kuwa vijana walioajiriwa watakaoanza uzalishaji huo ni wahitimu kutoka vyuo mbalimbali nchini na wamepewa mafunzo maalum ya uzalishaji huo.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa hadi sasa dola za kimarekani milioni moja zimewekezwa kwa ajili ya kuanza uzalishaji wa vishikwambi, kompyuta mpakato na projekta.

"Hiki ni kiwanda cha kwanza nchini ambacho kitakuwa kinatengeneza bidhaa hizi na bei zetu zitakuwa nafuu. Bidhaa zetu zitakuwa na viwango vya juu vya kukidhi vigezo vya kimataifa," alisema.

Alifafanua kuwa projekta imetengenezwa kwa lengo la kusaidia mafunzo kwa njia ya mtandao ili kuondokana na matumizi ya vitabu shuleni.

"Projekta hizi walimu wanaweza kuzitumia bila umeme, hivyo zinatumika mahali popote. Zimetengenezwa kwa viwango vya juu na zina hadi kamera. Hii ni nzuri. Inapunguzia serikali gharama za kuchapisha vitabu kila mwaka," alisema.

Mkurugenzi huyo pia alisema kiwanda kitatumia baadhi ya malighafi za ndani na nje ya nchi.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema kampuni hiyo itaanza uzalishaji mwezi huu na kuwahamasisha Watanzania kununua bidhaa hizo kwenye soko la ndani badala ya kuagiza nje ya nchi.

Prof. Mkenda alisema serikali ilipa masharti matatu kampuni hiyo ikiwamo programu ya kuanza kuwafundisha Watanzania mambo ya uhandisi wa kielektroniki.

"TANZTECH wanatarajia kuanza kuzalisha vishikwambi nchini na moja ya masharti ni kuunganisha vifaa mbalimbali na kutoa tablets (vishikwambi) na wanaanza mkakati wa kuzalisha hizo pads na si tu kuchukua baadhi kutoka China na kwingineko. Baadhi ya bidhaa zitazalishwa hapahapa nchini," alisema.

Prof. Mkenda alisema kampuni hiyo itaungana na serikali kwenye vyuo vyake vya ufundi vya VETA, DIT, Arusha Tech kuwasaidia wanafunzi kuingia kwenye mafunzo maalum wa mambo ya kielektroniki na uhandisi wa kielektroniki.





# Viongozi TALGWU wasimamishwa kazi kisa maadhimisho ya Mei Mosi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) Mkoa wa Mbeya, kimewasimamisha kazi viongozi wake katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili.

Viongozi hao wanatuhumiwa kuwatelekeza wanachama wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani ambayo kimkoa yalifanyika katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Waliosimamishwa ni Mwenyekiti wa chama hicho Wilaya, Emmanuel Dalika na Katibu wa chama hicho, Joyce Amelye ambao wanadaiwa kuwatelekeza wanachama walioshiriki maonyesho hayo bila kuwalipa posho na kuwapatia chakula.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi ofisini kwake, Mwenyekiti wa TALGWU Mkoa wa Mbeya, Lugano Bansilile, alisema viongozi hao hawakuwa na mawasiliano mazuri na wanachama na ndiyo sababu wanachama hao walikuwa wanalalamika.

Pia alidai waliwatukana wanachama waliokuwa na madai mbalimbali kwenye uwanja wa maonyesho, jambo ambalo lilisababisha vurugu baina yao na wanachama. Vilevile, alisema viongozi hao wanatuhumiwa kuwatoroka wanachama na wakazima simu. Hata walipotafutwa na viongozi wa mkoa, hawakupatikana.

"Tumeamua kuwasimamisha kazi ili tufanye uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili. Kwa kawaida huwezi ukawa unamchunguza mtu wakati anaendelea kutumikia nafasi ileile, anaweza asikupe ushirikiano mzuri," alisema Bansilile.

Akizungumzia jambo hilo, aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho wilaya, Dalika alikana kauli ya mwenyekiti wa mkoa ya kumsimamisha kwa maelezo kuwa yeye aliamua kujiuzulu mwenyewe kwa hiyari baada ya kudhalilishwa na baadhi ya wanachama.

Alisema siku ya maadhimisho, yeye ni miongoni mwa maofisa waliokuwa wamekaa jukwaa kuu na hakuziona simu za wanachama ambao walikuwa wanampigia na kwamba alikuwa hasikii zikiita kutokana na kelele.

Alisema baadaye mmoja wa wanachama, Richard Mgogo alimfuata jukwaani na kwenda kumvuta na kushuka naye mpaka walikokuwa wanachama wengine ambao walikuwa wanataka posho na chakula.

Alisema kutokana na kutoelewana, Mgogo alianza kumtukana na kumpiga jambo ambalo lilimfanya achukue uamuzi wa kujiuzulu ili kuepusha mgogoro huo kuendelea na hata kusababisha ugomvi miongoni mwao. "Mimi siyo mwajiriwa wa TALGWU, bali ni mwajiriwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, huku unachaguliwa na wanachama baada ya kuridhika na sera zako. Kwa hiyo, nimeamua kujiuzulu nafasi zangu zote ndani ya chama hiki kwa sababu nimedhalilishwa," alisema Dalika.

Aliuomba uongozi wa TALGWU mkoa pamoja na viongozi wa serikali katika wilaya ya Mbeya kuzungumza na Mgogo ili aache kujichukulia sheria mkononi.

Mgogo ambaye ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ikukwa alidai viongozi wao hao walikuwa ni jeuri na waliwatukana matusi wakati wanawahoji kuhusu vitu ambavyo walikuwa wamewaahidi.

Alidai mwenyekiti wao aliwaahidi kwamba angewaandalia chakula lakini walipofika kwenye eneo walilokuwa wameelekezwa, hawakukuta chakula, jambo ambalo liliwazidishia hasira.

Mgogo alisema kuwa kwenye maadhimisho hao, washiriki kutoka katika halmashauri zingine zote walilipwa posho isipokuwa wao.

Mei Mosi mwaka huu zaidi ya wanachama 70 wa TALGWU kutoka Wilaya ya Mbeya ambao ni watendaji wa vijiji na kata, maofisa kilimo na maofisa wa afya kutoka katika halmashauri hiyo waligoma kutoka uwanjani wakishinikiza walipwe posho.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka (wa pili kushoto), akikagua tumbaku iliyohifadhiwa kwenye moja ya maghala katika Kata ya Lupatingatinga, alipokuwa akizindua masoko ya zao hilo juzi. Kushoto ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Ununuzi wa Tumbaku ya Mkwawa, Ahmed Huwel. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## CCM yaahidi ushirikiano kulinda uhuru wa habari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimeahidi kuendelea kushirikiana na waandishi wa habari kulinda uhuru wa vyombo vya habari ili kuendelea kukuza taaluma hiyo.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho Taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alitoa ahadi hiyo juzi alipozungumza kuhusu miaka 30 ya maadhimisho ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani.

Alisema chama hicho kitaendelea kulinda uhuru wa habari kwa sababu ni miongoni mwa vitu ambavyo vimeainishwa kwenye Ilani yake ya uchaguzi ya chama hicho ambayo inatekelezwa sasa hivi.

Alisema chama hicho kinavitumia vyombo vya habari kama tochi za kumulika baadhi ya maeneo ambayo hakiwezi kuyafikia pamoja na kuvitumia kutangaza mambo mazuri ambayo kinatekeleza. Mwaselela alisema chama hicho kitauelekeza uongozi wa mkoa huo kuhakikisha unaondoa vikwazo vidogo ambavyo vimekuwa vikiwakabili wananchi.

"Rais wetu ameonyesha mfano katika kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari. Alipoingia madarakani, moja ya vitu alivyovifanya ni kuvifungulia vyombo vilivyokuwa vimefungiwa kwa muda mrefu. Kwa hiyo, lazima na sisi wasaidizi wake tuige kuruhusu uhuru," alisema Mwaselela.

Aliwaomba waandishi wa habari kuendelea kufanya kazi kwa uhuru na kufuata misingi ya taaluma hiyo ili wawahudumie wananchi vizuri.

Aliwaomba wamiliki wa vyombo vya habari kuendelea kuajiri watu ambao wamesomea taaluma hiyo badala ya kuajiri watu wasiokuwa na taaluma ambao ndio wanaharibu taswira ya taaluma.

# Wabainika kuchanganya taka kwenye tumbaku

**Na Mwandishi Wetu,** CHUNYA

BAADHI ya wakulima wa tumbaku katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wamebainika kuchakachua tumbaku kwa kuchanganya na taka ili kuongeza uzito, jambo ambalo linashusha ubora wa tumbaku na kuharibu soko.

Meneja wa Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku Chunya (CHUTCU), Juma Nshishi, alibainisha hayo juzi wakati wa uzinduzi wa masoko ya tumbaku wilayani humo uliofanyika Kata ya Lupatingatinga wilayani hapa.

Alisema msimu uliopita baadhi ya wakulima wa Chama cha Msingi cha Igangwe walichanganya tumbaku yao na uchafu, jambo ambalo liliwashtua wanunuzi. Wakalazimika kuwaita viongozi kwenda kuhakiki mkoani Morogoro.

Alisema ili kuhakikisha zao hilo linaendelea kuwa na soko zuri, ni vyema wakulima wakawa wanachambua vizuri majani, wanaanika vizuri na kufungasha bila kufanya uhuni wa aina yoyote.

"Tunatakiwa tuepuke kuwakatisha tamaa wanunuzi wetu. Tuache kuchanganya na uchafu kama ambavyo ilitokea msimu uliopita ambapo ofisa kilimo wetu alilazimika kwenda mkoani Morogoro kuhakiki," alisema Nshishi.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya ambaye ndiye alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa masoko hayo, Mayeka Simon, alisema udanganyifu ambao umekuwa unafanyika kwenye tumbaku "ni wa kijinga kwa kuwa ni rahisi kubainika".

Alisema kuwa baada ya ofisa kilimo kwenda kuhakiki tumbaku iliyokuwa imechafuliwa mkoani Morogoro, wahusika walibainika na kuchukuliwa hatua mbalimbali na hivyo akawataka wakulima wengine kuacha kufanya hivyo.

Alisema wanapochanganya na uchafu, wanasababisha wanunuzi wawe na wasiwasi na tumbaku inayolimwa wilayani hapa na hivyo kuanza kuiepuka, hali ambayo itawaumiza wao wenyewe kwa kukosa soko la uhakika.

Alisema kitu ambacho kimekuwa kikiwasukuma wakulima hao kuchakachua na uchafu ni tamaa ambazo aliziita za kijinga pamoja na tabia ya ubinafsi miongoni mwa wakulima hao ambao wanataka kujinufaisha wao wenyewe.

"Tusikubali kuharibu soko la zao letu kwa sababu ya ujinga wa watu wachache, unapochafua tumbaku kwenye mitumba ni ujinga kwa sababu utabainika, hii ni sawa na kenge anajificha kichwa lakini mwili mzima unaonekana," alisema Mayeka.

Baadhi ya wakulima walishukuru serikali kwa kushawishi kampuni nyingi kuingia wilayani hapa kununua tumbaku wakidai kuwa imesaidia kuongeza ushindani ambao umesaidia madaraja na bei kupanda tofauti na ilivyokuwa awali.

Mmoja wa wakulima hao, Jonas Njeyo, alisema misimu iliyopita walikuwa na kampuni chache zilizokuwa zinanunua zao hilo, hapakuwa na ushindani wa bei.

# Zanzibar kunufaika zaidi mazao bahari

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema ina nia ya dhati ya kunufaika zaidi na matunda ya baharini kupitia sera yake ya uchumi wa buluu kwa kuvuna mengi zaidi kuliko inavyoendelea sasa ili kuimarisha uchumi wa nchi.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Balozi wa Canada nchini Tanzania, Kyle Nunas, aliyefika kumtembelea.

Alisema kupitia uchumi wa buluu, Zanzibar pia inanufaika na biashara kupitia bahari kwa mipaka jirani ya Dar es Salaam, Tanga, Mombasa na visiwa jirani vikiwamo vya Comoro.

Rais Dk. Mwinyi alimweleza balozi huyo kwamba utalii ni sekta namba moja ya uchumi wa Zanzibar na kwamba serikali imejikita kuimarisha miundombinu yote ikiwamo ujenzi wa bandari jumuishi ya Mangapwani ambayo itatoa fursa zaidi za uchumi, kupanua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kwa kuongeza jengo jipya la nne la (Terminal 4), kuboresha barabara, kuongeza hoteli za kisasa na nyumba za wageni na kuimarisha vivutio vya utalii.

Dk. Mwinyi alisema Zanzibar kwa sasa inapokea ndege nyingi za kimataifa kiasi cha kuongeza idadi kubwa ya watalii nchini.

Pia alisema serikali ina nia ya kulifufua eneo kongwe la hoteli ya Bwawani kwa kujengwa kumbi kubwa za mikutano kwa ajili ya watalii ili kuongeza mapato ya nchi.

Kuhusu sekta za afya na elimu, Rais Dk. Mwinyi alimweleza balozi huyo kwamba serikali pia inaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma bora hasa kwenye maeneo ya vijijini ili kujenga uwiano sawa wa huduma na sehemu za mijini.

Katika afya, Rais Mwinyi alisema serikali inazingatia kukuza huduma ya afya ya kinga kwa mama na mtoto na mapambano dhidi ya magonjwa ya kuambukiza.

Alisema uhusiano wa diplomasia baina ya Tanzania na Canada ni wa muda mrefu pia Zanzibar ikiwa sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefaidika na uhusiano huo hasa kupitia sekta za afya na elimu.

Balozi Nunas ameisifu Tanzania ikiwamo Zanzibar kwa kubarikiwa kuwa na amani na utulivu na siasa za kistaarabu katika kuimarisha ustawi wa nchi.

Nunas alisema Canada inaunga mkono zaidi masuala ya haki za binadamu hasa kwa makundi maalumu wakiwamo wanawake na wasichana na kwamba imeelekeza sera na miradi mingi kwenye eneo hilo.

Alisema Canada imevutiwa zaidi na ustaarabu wa Tanzania hasa katika kuimarisha demokrasia, uhuru wa vyombo vya habari na alimweleza Dk. Mwinyi kwamba nchi yake inavutiwa kuiona Tanzania inavyoendeleza siasa za kistaarabu na mazungumzo ya busara kwa kambi pinzani.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiongoza kikao cha Baraza la Mapinduzi, Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Waziri akiri uwezeshaji mdogo wanawake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amesema kuna umuhimu wa kutambua kuwa pamoja na maendeleo ya sera, mifumo ya kisheria inayohimiza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake katika sekta za umma ikiwamo ya nishati bado ni mdogo.

Pembe aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa mpango wa uendelezaji wa uwezo wa watendaji wanawake (ZESTA) na uwekaji saini wa mkataba wa maelewano baina ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na taasisi za elimu ya juu.

Alisema ushiriki wa wanawake katika sekta ya nishati ni muhimu kwa sababu sekta hiyo ina mchango mkubwa katika kusaidia na kukuza mabadiliko ya uchumi wa nchi.

Pia alisema utafiti unaonyesha kuwa tofauti za kijinsia katika uamuzi ya ngazi ya juu huhusiana na utendaji bora, unaonyesha kwamba kampuni zenye wanawake wengi zaidi kwenye ngazi za juu za uongozi hufanya vyema zaidi.

Alisema pengo hilo la usawa wa kijinsia linachangiwa na ukosefu wa usawa wa kupata elimu, uelewa mdogo na ufinyu wa wanawake katika fani za ufundi na fursa za kimafunzo.

Waziri Pembe alisema kutokana na hali hiyo, kuna umuhimu wa kuwatambua wanawake kama wahusika wakuu wa masuala ya nishati na kutambua uwezo wao wa kushiriki rasmi kama wafanyakazi, watoa uamuzi na katika mnyororo wa thamani.

Alisema hatua hiyo itapelekea kuongezeka kwa fursa za wanawake katika nyanja za kiuchumi na uwekezaji katika sekta ya nishati. Kwa mujibu wa Pembe, mpango wa ufadhili wa masomo kwa walio kazini utasaidia wafanyakazi wa kike kuboresha sifa zao za kitaaluma na kuendeleza ujuzi wao mwingine kwa ajili ya maendeleo ya kazi na kupata nafasi nzuri ikiwamo fursa za kuteuliwa katika nafasi za uongozi.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Mwanajuma Majid Abdullah, alisema ZESTA ni mradi wa miaka sita unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na unalenga kuboresha miundombinu ya umeme, kuongeza ubora wa huduma za umeme na kuongeza kiwango cha umeme kwa kutumia nishati mbadala Zanzibar.

Alisema mradi huo una thamani ya Dola za Marekani milioni 142 na unatekelezwa na taasisi tatu ambazo ni Idara ya Nishati na Madini, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA).

Mwanajuma alisema mradi huo utawanufaisha wananchi wa Zanzibar hasa katika uongezaji wa nishati ya umeme kwa kupatikana kwa nishati ya umeme wa jua hasa vijijini.

Naye mwakilishi wa mambo ya usawa wa kijinsia kutoka Benki ya Dunia, Meskerem Mulatu, alisema licha ya serikali nyingi kuwajali wanawake katika ngazi za ufanyaji wa kazi, bado katika mashirika ya nishati za umeme imekuwa changamoto kuwakuta wanawake wanafanya kazi huko. Alisema mradi huo unatarajia kuwa mkombozi kwa wanawake katika kuzidisha idadi ya wafanyakazi kupitia ZECO kwa Zanzibar na hiyo ndiyo shabaha ya Shirika la Fedha Duniani .

# Waziri ataka viwango ujenzi wa kituo mabasi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, ameitaka kampuni ya CRJE Tanzania iliyopewa kazi ya kujenga kituo cha mabasi katika eneo la Kijangwani kuzingatia viwango na kukamilisha mradi huo ndani ya wakati uliopangwa.

Dk. Khalid alitoa agizo hilo jana aliposhiriki na kushuhudia utiaji saini wa ujenzi wa kituo hicho katika hafla iliyofanyika Kariakoo, mjini Zanzibar.

Utiaji saini huo uliwakilishwa na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Nassor Shaaban Ameir na Meneja wa CRJE, Xu Chang.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa utiaji saini huo, Waziri Dk. Khalid aliipongeza ZSSF kwa uthubutu na ubunifu wa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Aidha, aliutaka uongozi wa ZSSF kusimamia kwa karibu ujenzi wa kituo hicho kwa kuteua mshauri elekezi atayekasimamia kwa upande wa serikali na kuhakikisha ujenzi huo unakamilishwa kwa viwango vinavyotakiwa.

Waziri Dk. Khalid pia alisema ZSSF itarejesha historia kwa kukijenga kituo cha mabasi katika eneo hilo na miaka ya 1970 eneo hilo lilikuwa likitumiwa kwa shughuli kama hizo.

Naye Ameir alisema ZSSF imeamua kujikita katika ujenzi wa vituo vitatu vya mabasi kwa hatua ya awali lengo likiwa ni kutatua changamoto na kuwaondoshea usumbufu wananchi katika huduma ya usafiri.

Alisema vituo hivyo vitajengwa katika eneo la Kijangwani, Malindi na Mnazi Mmoja huku wakisogeza huduma ya ujenzi wa vituo hivyo nje ya mji kulingana na uhitaji.

Chang alisema kampuni yake itahakikisha inajenga kituo hicho katika ubora unaotakiwa na kumaliza kwa wakati uliopangwa na wanakusudia kuingiza vifaa vya ujenzi vya kisasa katika kutekeleza kazi hiyo ya ujenzi.

Ujenzi wa kituo hicho unatarajiwa kugharimu jumla ya Sh. 8,670,449,321.21 na kinakadiriwa kuwa na maduka 78, sehemu sita za huduma za kutolea fedha, chakula na huduma za vyoo. Ujenzi huo unatarajia kukamilika ndani ya miezi 10.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**RAINFRIDA CHESCO MLIGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S3641-0010** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NABOTI SEKONDARI** mwaka **2018.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MKB/RB/1635/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**REHEMA WILLIAM MWAMBENJA,**

Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 850 AZX** Chassis namba **JTZ53AE000044382** Engine namba **SAC094203** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi:-

**DAR/URA/RB/146252/2023**

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. ......../2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**BENEDICT LUBIGA KAMAGI WA KIVULE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**
**MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ZUNDA ISSA DOGRAS**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 29 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 28 Mwezi wa 04 Mwaka 2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA TRACTOR

**JANE JAPANDA SANGA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya Tractor Ford yenye namba za usajili **T 390 AJS. CHASSIS NO. A73422. ENGINE NO. 876049.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**ARU/ARU/RB/153825/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**SITA SENGEREMA** Pichani anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye Index namba CS 110158874 kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia TALLO SECONDARY SCHOOL mwaka 2011. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

**Taarifa ya polisi. MW/RB/2140/2014**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **CRESCENTIUS JOHN MAGORI** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 717 DLK.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KW/RB/2073/2023** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARY SAPHENATH MANGESHO**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 361 DUK** - TOYOTA ALLEX. CHASSIS NO. **NZE1210065129.** ENGINE NO. **INZA224082.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/153675/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA TRELA

**PTL ROAD WAYS LIMITED**

anatangaza kupotea kwa kadi ya Trela yenye namba za usajili T 612 CPL. Chassis namba 27697. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya **polisi:**

**DAR/URA/RB/168897/2023.**

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 664/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**NIRMALABEN BHAGWANJI NADIADHARA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA BHAVESH YOGESH NADIADHARA**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 04 Mwezi wa 05 Mwaka 2023.

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya**
**DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 30/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ZAINAB SAID ISMAIL wa Chang'ombe**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA**
**NA FATUMA ALLY REUBEN**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 04 Mwezi 05 Mwaka 2023.

04 05 2023

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO-MJINI DODOMA

**SPECTRA AUTO SOLUTIONS LIMITED**
**COMPANY NO: 138410765**
**AT EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING OF BOARD OF THE MEMBERS OF THE COMPANY HELD AT THE REGISTERED OFFICE ON 25TH DECEMBER, 2022.**
**THE FOLLOWING SPECIAL RESOLUTION WAS DULY PASSED AND ADOPTED, NAMELY;**
**SPECIAL RESOLUTION:**

- It was RESOLVED that the Company be wound up voluntarily under sections 334 and 335 of the Companies Act, 2002 as proposed by the Directors of the Company which took effect from 25th day of December, 2022.
- It was RESOLVED that Legalsure Attorneys of P.O. Box 10233, Dar es salaam be appointed as liquidator of SPECTRA AUTO SOLUTIONS LIMITED for the purpose of winding up the company's affair and distributing its assets if any.
- It was RESOLVED that Liquidator published the notice of winding up the company voluntarily by the members in the newspaper of Mwananchi and Daily News and Government Gazette.
- It was further RESOLVED that Liquidator has furnished the report and final accounts of the Company before the members.
- It was further RESOLVED that members be informed of this development and the necessary documents to this effect, be prepared, signed and filed with the Company registry.

IT IS HEREBY CERTIFIED that the above was duly passed in accordance with and complied with the Memorandum and Articles of Association.

Dated and signed at Dar es salaam this 25th day of December, 2022.

..........................
**Chairperson**
**Company Secretary**
**SPECTRA AUTO SOLUTIONS LTD**
**P.O. Box 8648**
**DAR ES SALAAM.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**JAMES IBRAHIM SHEMDOE** anatangaza kupotelewa na cheti cha Diploma ya Ualimu chenye index namba E0506/069 kilichotolewa na Chuo cha Ualimu Marangu mwaka 1992. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MTW/MTW/RB/142410/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya MOROGORO Kituo cha KIHONDA Mkoa MOROGORO**
**Shauri la Madai / Ndoa Na...../2023**

**Jina la Mdai: Mkombozi Osward Sauli**
**Jina la Mdaiwa: Farida Rajabu Mbilikila**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya (18) ya kanuni za taratibu za madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa FARIDA RAJABU MBILIKILA**
**KILAKALA MOROGORO**
**Kwa kuwa mdai / Wadai ameleta / Wameleta Madai yake / yao kwamba (Eleza hapa habari za madai)**
**TALAKA NA MATUNZO YA MTOTO MMOJA**

Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe **8 mwezi 5 mwaka 2023** Saa 2;30 Asubuhikwa mujibu wa madai hayo vielelezo vyote vinavyohusu madai hayo kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautoudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolwa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe **4/5/2023**

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA MOROGORO


**OFISI ZA MATANGAZO**

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0677020701

E-mail: advertise@guardian.co.tz,

Website: www.ippmedia.com

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Ukabila, udini wahusishwa vita Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

UKABILA na udini unadaiwa kuhusika katika mgogoro wa kivita unaoendelea kati wa majenerali wawili wa jeshi la Sudan Abdel Fattah al-Burhan na makamu wake, Mohamed Hamdan Daglo, wa kikosi cha Rapid Support Forces (RSF).

Inaelezwa kuwa majenerali hao wanagombania madaraka na maslahi ya kiuchumi hususani umiliki wa mali asili za nchi hiyo iliyopo kaskazini mashariki mwa bara la Afrika.

Wataalamu wa masuala ya migogoro na baadhi ya wanaharakati wa muungano wa makundi ya kiraia nchini Sudan ambao hawakutaka majina yao yatajwe wakihofia usalama wao, waliiambia VOA kuwa mgogoro huo uliozuka ghafla wiki mbili zilizopita una historia inayoonyesha kuwapo kwa misingi ya ukabila na udini.

**Ukiwa katika makao makuu Khartoum mapigano yanaonekana kuwa ni ya kati ya RSF na Jeshi la Sudan, na ukiwa eneo la Magharibi yanaonekana ni kati ya Waafrika na Wasudan wenye asili ya Kiarabu.**

Prof. Dan Rothbath wa shule ya utatuzi wa migogoro katika chuo kikuu cha George Mason Marekani, alisema kwa kawaida vipengele vya migogoro yenye misingi ya udini au ukabila huwa havihusishwi moja kwa moja kuwa ni chanzo cha mgogoro.

Naye mkurugenzi wa Kituo cha Orfalea cha Masomo ya Kimataifa kilichopo katika Chuo Kikuu cha California tawi la Santa Barbara Prof. Mark Juergensmayer alisema "Kijuu juu inaonekana kama ni vita kati ya RSF na SAF wakati inajulikana uasili wa RSF unatokana na wanamgambo wa Janjaweed ambao wanashukiwa walihusika katika mauaji ya kikabila huko Darfur".

Micheal Beer, ambaye ni mkurugenzi wa shirila la Non violence International lililopo Washington DC, alisema mgogoro huo unatazamwa tofauti kulingana na eneo.

"Ukiwa katika makao makuu Khartoum mapigano yanaonekana kuwa ni ya kati ya RSF na Jeshi la Sudan, na ukiwa eneo la Magharibi yanaonekana ni kati ya Waafrika na Wasudan wenye asili ya Kiarabu," alisema.

Akielezea uasili wa mikoa wanakotoka wanajeshi wa makundi hayo yanayohasiana, Mubaraka El Amin mkazi wa jiji la Seattlle huko Washington, alisema kuwa wanajeshi wengi wa RSF wanatoka eneo la magharibi lenye mchanganyiko wa makabila ya Afrika Magharibi kama vile Niger, Mali na Chad.

Alisema kwa upande wa wanajeshi wa Sudan wanatoka eneo la Kaskazini mwa nchi hiyo, jeshi ambalo pia lina mahusiano na viongozi wa ngazi za juu wa utawala uliopita walioondolewa madarakani mwaka 2019.

"Bashir ni mlezi (Godfather) wa majenerali wote wa jeshi," alisema mwanaharakati wa kisiasa kutoka muungano wa mashirika ya kiraia ya Khartoum, akieleza kuwa dini inatumiwa na wanachama wa 'Muslim Brotherhood' katika jeshi kupata uhalali wa kisiasa.

Wizara ya Mambo ya Nje mjini Juba, Sudan Kusini ilisema katika taarifa yake kwamba majenerali hao wawili wamekubaliana kimsingi kusitisha mapigano kwa siku saba kuanzia Mei 4 hadi 11 mwaka huu. **VOA**




Wananchi wakiopoa vitu vyao baada ya mafuriko kuyakumba baadhi ya maeneo nchini Rwanda, juzi. **PICHA: REUTER**

## Zelensky ataka Rais Putin ahukumiwe

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, ametoa wito wa kuanzishwa kwa mahakama maalum ambayo itaiwajibisha Russia kutokana na makosa ya uvamizi iliyoufanya Ukraine.

Rais Zelensky, pia aliishutumu Russia kwa matukio ya uhalifu wa kivita 6,000 mwezi Aprili pekee na kusababisha vifo vya raia 207 wa Ukraine wakiwamo watoto 11.

Pia aliorodhesha uhalifu mwingine wa kivita unaodaiwa kufanywa na Russia ikiwamo mamilioni ya mashambulizi katika mikoa ya Donbas na wale waliouawa wakati ilipokuwa imekalia eneo la Bucha.

Alisema wote wanataka kuona Vladimir tofauti, huku akimuashiria Rais Putin, ambaye alimuita anayestahili kuhukumiwa kwa vitendo vya uhalifu katika mji mkuu wa sheria za kimataifa.

Aliishukuru Uholanzi kwa kutoa silaha kwa Ukraine, na kwamba vita vinashindwa kwa nguvu ya silaha, huku akitilia mkazo wito wake wa mara kwa mara wa kutaka silaha zaidi kutoka kwa washirika wake.

"Mzozo wa Ukraine ulikuwa ni vita ambavyo hatukuvitaka, vita ambavyo tunapaswa kuvifanya vya mwisho na tutafanya hivyo," alisema.

Wakati hayo yakiendelea, Russia nayo imeishutumu Marekani kwa madai ya kuhusika na shambulizi la ndege zisizo na rubani kwenye Ikulu ya Kremlin, na kwamba ilikusudia kumuua kiongozi wa taifa hilo.

Msemaji wa Kremlin Dmitry Peskov, alidai kwamba maamuzi juu ya mashambulizi hayo hayafanywi mjini Kyiv, bali Washington.

"Kyiv hufanya tu kile inachoambiwa kufanya," aliwaambia waandishi wa habari katika mkutano mfupi.

Hata hivyo, Peskov hakutoa ushahidi wowote kuunga mkono madai hayo, lakini alisema kuwa uchunguzi wa dharura unaendelea. **BBC**

## Vifo vyafikia 127 mafuriko Rwanda

**KIGALI,** Rwanda

IDADI ya vifo imefikia 127 nchini Rwanda, baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mafuriko na maporomoko ya udongo, Magharibi na Kaskazini mwa nchi hiyo.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya ndani, mafuriko hayo yalitokea usiku wa kuamkia juzi, na kwamba maeneo ya Magharibi hasa Rutsiro, ndiyo yaliyoathiriwa zaidi, huku kukiwa na wasiwasi kuwa huenda idadi ya maafa ikaongezeka baada ya baadhi ya watu kutojulikana waliko.

Wataalamu wa hali ya hewa wanatabiri kuwa mvua kubwa itaendelea kunyesha nchini Rwanda mwezi huu.

"Kumenyesha mvua kubwa, kuna mito ambayo kingo zilivunjika na kukawa na maporomoko ya udongo ambayo yalisababisha maafa makubwa," alisema Emmanuel Mazimpaka ofisa wa Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Rwanda.

Naibu msemaji wa serikali ya Rwanda, Alain Mukuralinda, alisema juhudi za kuwatafuta watu waliopotea na kuwaokoa walio hai zinaendelea baada ya kutokea mafuriko na maporomoko ya udongo, Magharibi na Kaskazini mwa nchi hiyo.

"Kuna mto uliovunja kingo zake kutokana na mvua kubwa na maji yakateremka hadi kwenye barabara yenye lami, mimi naliita tukio hili kama janga la asilia," alisema Mukuralinda. **RFI**

# COSMOPOLITAN BINGWA FIRST LEAGUE 2022/2023

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara mwaka 1967, Cosmopolitan wamefanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Daraja la Pili 'First League' msimu huu baada ya kuibamiza Stand United kutoka Shinyanga mabao 3-1 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi.

Timu zote hizo mbili zimepanda daraja na msimu ujao zitacheza Ligi ya Championship baada ya kutinga hatua ya fainali ya ligi hiyo ambayo awali ilianza kuchezwa kwa makundi mawili, kila timu likiwa na timu nne.

**Zote zilikuwa Kundi A, Stand United ilitoka kinara ikiongoza kwa pointi sita, Cosmo ikimaliza ikiwa ya pili kwa pointi nne, katika kundi lao wakiwa pamoja na Lipuli ya Iringa na Alliance FC ya jijini Mwanza.**

Cosmopolitan ilianza kuandika bao lake la kwanza kupitia kwa Amasi Ally dakika ya 10 kabla ya vigogo hao wa Shinyanga, Stand United kusawazisha dakika saba baadaye, goli lao likiwekwa ndani ya vyavu na Kimu Juma.

Hadi mapumziko, timu hizo zilikuwa sare ya bao 1-1.

Bao la pili la washindi lilifungwa dakika ya 49 na Benjamin Dominick, kabla ya mchezaji huyo kupigilia msumari wa mwisho dakika ya 61, alipopachika goli la tatu lililowahakikishia ubingwa.

Kabla ya mechi hiyo, kulitanguliwa mechi ya kusaka mshindi wa tatu wa ligi hiyo, Dar City ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya TMA FC.

Timu hizo ziliingia nusu fainali kutoka Kundi B, lakini hakuna hata moja iliyofanikiwa kuingia fainali, badala yake ziliishia katika hatua hiyo.

Dar City ambayo imemaliza ligi hiyo ikiwa ya tatu ilifungwa mabao 2-1 dhidi ya mabingwa wapya, Cosmopolitan katika mechi ya nusu fainali, na TMA ilitolewa kwa mabao 2-1 na Stand United, mechi ikichezwa dakika 120, baada ya kumaliza dakika 90 kwa sare ya bao 1-1.




Mchambuzi wa soka nchini, Abubakary Liongo (kushoto), akitoa maoni yake kuhusu Ligi Kuu England inavyoenda. Wengine pia ni wachambuzi wa mchezo huo, Geofrey Lea (kulia), Jemedari Saidi na Edgar Kibwana walipokuwa katika hafla fupi ya uzinduzi wa Kampeni ya TV ni DStv iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DStv sasa yaja na TV ni DStv

**Na Mwandishi Wetu**

MAMBO yanazidi kunoga ndani ya DStv huku ligi na mashindano makubwa ya soka hususan barani Ulaya yakielekea ukingoni.

Katika kuhakikisha mteja wa DStv hakosi kila aina ya burudani, kampuni hiyo imejipanga kuhakikisha wateja wao wanapata kila aina ya burudani kulingana na mahitaji huku ikiendelea kutoa ofa maalum kwa wateja wapya kujipatia seti nzima ya DStv kwa Sh. 99,000 hii ikijumuisha na kifurushi cha Compact cha Sh. 56,000 bure.

Kaimu Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Shumbana Walwa, amesema DStv imeongeza burudani kiasi kwamba unapozungumzia TV, unamaanisha DStv kwani ndipo zinapopatikana kila aina ya vipindi ikiwamo burudani, michezo, filamu, Habari, Makala na vipindi motomoto vya Watoto.

"Tunaposema TV ni DStv, tunamaanisha sasa mteja mwenye DStv nyumbani kwake anapata vipindi vya kila aina tena kwa gharama nafuu kulingana na uwezo wake, sasa vifurushi vyetu vinaanzia Sh. 10,000 tu!"

Ametoa mfano kwa wapenzi wa soka ambapo wataendelea kushuhudia michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika ambapo Yanga imetinga nusu fainali, michuano ya ligi maarufu duniani kama EPL, La liga na Serie A bila kusahau michuano ya UEFA, EUROPA League, FA na mingineyo.

Pia mashabiki na wapenzi wa michezo mingine nao hawajaachwa nyuma kwani michezo ya kikapu (NBA), Formula One, mieleka, ngumi, tenisi, rugby, kriketi na mingineyo bado inaonekana kwenye kisimbuzi cha DStv.

Shangwe kubwa ni kwa wale wapenzi wa filamu za Bongo ambapo tamthilia maarufu kama Jua kali, Huba, Pazia bado zinazidi kupamba moto bila kusahau vipindi vingine kama Mwali, Mizani ya Ushambenga, Kitimtim, ICU, Ya Walimwengu Pamoja na vichekesho vya Orijino komedy na Watu baki vikiwa vinaendelea.

Naye Mkuu wa Huduma kwa Wateja wa DStv Tanzania, Davis Mihayo, amesema mbali na kuwahakikishia wateja wa DStv burudani wamejipanga kuwahudumia wateja kwa ufanisi mkubwa zaidi.

## TFS yaandaa mbio katika Msitu wa Sao

**Na Beatrice Shayo**

WAKALA wa Misitu Tanzania (TFS) umetangaza zao jipya la utalii ambalo ni mbio za magari zitakazozinduliwa kati ya Mei 13 na 14, mwaka huu ndani ya Msitu wa Sao uliopo mkoani Iringa, imefahamika.

Mhifadhi na Mkuu wa Sehemu ya Kutangaza Utalii Ekolojia wa TFS, Anna Lawuo, alisema tayari washiriki kutoka ndani na nje ya Tanzania wameshaanza kujiandikisha.

"Tumekuja na zao jipya la utalii la kuendesha magari ndani ya msitu. Tuna misitu takribani 24 ambayo inasifa ya kuwa na mbio za kuendesha magari, pikipiki, baiskeli na wanaokwenda kwa miguu, hili eneo linafaa kwa utalii wa ekolojia," alisema ofisa huyo.

Aliongeza TFS watashirikiana na CMC Automobiles Sao Hill Forest Rally wa Iringa katika kufanikisha mbio hizo zitakazowapa pia fursa washiriki kutembelea misitu.

Naye Mwenyekiti wa Klabu ya Magari ya Mkoa wa Iringa, Amjad Khan, alisema wanaishukuru TFS kwa kuwapatia maeneo kwa ajili ya kuendeleza mchezo huo ambao utasaidia katika kutangaza utalii nchini.

## Uhamiaji FC yatupwa nje Kombe la ZFF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAAFANDE wa Uhamiaji FC wameondolewa katika mashindano ya Kombe la FA Zanzibar (ZFF FA Cup) baada ya kufungwa penalti 4-2 na Mwembe Makumbi City katika mechi ya hatua ya 16 bora iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau ze Don juzi.

Timu hizo zililazimika kufika hatua ya matuta baada ya dakika 90 za kawaida kumalizika wakiwa na sare ya mabao 2-2 na kufanya Uhamiaji kuwa timu ya pili inayoshiriki Ligi Ku kuondolewa katika michuano hiyo.

Kocha Mkuu wa Uhamiaji, Abdi Salehe, alisema jana matokeo hayo yamewaumiza kwa sababu waliamini wangesonga mbele katika mashindano hayo kutokana na maandalizi waliyofanya.

"Tumeumia sana, tulikuja kupambana kwa sababu tulihitaji kufanya vizuri katika michuano hii, tulikuja uwanjani na lengo la kupata ushindi na kusonga mbele katika michuano ya FA, lakini niseme haikuwa bahati yetu," alisema kocha huyo.

Mwembe Makumbi City inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda imeungana na KMKM, JKU, Mwembeladu, Dulla Boys na Mlandege FC kucheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ambayo bingwa hupata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MESSI KUMFUATA RONALDO

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi, 35, anaweza kumfuata mpinzani wake, Cristiano Ronaldo (38), kule Saudi Arabia kwa uhamisho wa pauni milioni 320 baada ya kuthibitisha anaondoka Paris St-Germain. ***(Telegraph)***

### MESSI AANZA KUGOMBEWA

KLABU ya Saudia ya Al-Hilal huenda ikaingia vitani kuwania saini ya Lionel Messi dhidi ya Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu Marekani, inayomilikiwa na nyota wa zamani wa Manchester United na England, David Beckham. ***(Guardian)***

### DORTMUND YAFUNGUKA

REAL Madrid ipo katika mazungumzo kuhusu kumnunua kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, 19, lakini klabu hiyo ya Ujerumani inasema bado haijapokea ofa kutoka kwa wababe hao wa Hispania. ***(Sky Germany)***

### SHEIKH JASSIM KUTIKISA

SHEIKH Jassim ameachana na mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Brazil Neymar, 31, ikiwa atafaulu kuinunua Manchester United, badala yake analenga kusajili nyota watatu wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 24 wa Paris St-German, Kingsley Coman wa Bayern Munich (26) na Eduardo Camavinga (20) wa Real Madrid ***(Bild's Christian Falk)***

### ARSENAL YAMTAKA DIABY

KIUNGO wa kati wa West Ham na England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24, mshambuliaji wa Bayer Leverkusen, Moussa Diaby (23) na nyota wa Crystal Palace, Wilfried Zaha (30) wa Ivory Coast na England, Marc Guehi, 22, ni miongoni mwa wachezaji wanaosakwa na Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta. ***(Mail)***

### ALONSO ATAJWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inamtaka kiungo wa kati wa zamani wa Liverpool na Hispania, Xabi Alonso, 41, kuwa mrithi wa Antonio Conte baada ya matakwa ya mshahara ya Julian Nagelsmann kuwatoa Spurs katika mbio za kumnasa Mjerumani huyo. ***(Metro)***

### WEGHORST: NITABAKI UNITED

MSHAMBULIAJI wa Uholanzi, Wout Weghorst, 30, ameonyesha nia ya kusalia Manchester United lakini Mashetani Wekundu bado hawajaanza mazungumzo na mchezaji huyo kuhusu kusalia Old Trafford wakati mkopo wake kutoka Burnley utakapoisha. ***(Telegraph)***

### ABRAHAM AGEUKA LULU

AS Roma inataka pauni milioni 35 kwa ajili ya mshambuliaji wa England, Tammy Abraham, 25. Manchester United, Tottenham na Paris St-Germain zinatarajiwa kupigana vikumbo katika dirisha lijalo la msimu wa joto kusaka huduma ya nyota huyo. ***(Calciomercato)***

### ZAHA ATAKIWA MARSEILLE

KLABU ya Ligue 1 ya Marseille itajielekeza kumsajili mchezaji wa Crystal Palace ambaye anamaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu, Wilfried Zaha ikiwa itafuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(FootMercato)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO MWANAMICHEZO ANAYELIPWA ZAIDI DUNIANI

**●●● Ni baada ya kukubali kutua Al Nassr ya Saudi Arabia kutokana na...**

**LONDON,** England

CRISTIANO Ronaldo amekuwa mwanamichezo anayelipwa kiasi cha juu zaidi cha fedha duniani kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2017 baada ya kuhamia Al Nassr ya Saudi Arabia.

**Forbes wameripoti mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno mwenye umri wa miaka 38 alipata Dola za Marekani milioni 136 katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.**

Mkataba wake na Al Nassr unaripotiwa kuwa na thamani ya zaidi ya euro milioni 200 kwa mwaka.

Ronaldo, nyota wa zamani wa Real Madrid ya Hispania aliamua kujiunga na Al Nassr baada ya kutokea kutoelewana na waliokuwa waajiri wake, Manchester United ya England.

Mreno huyo aliondoka huru baada ya kufanya mahojiano ambayo yaliharibu uhusiano wake na mabosi wake wa Old Trafford.

Nahodha wa Timu ya Taifa ya Argentina aliyeshinda Kombe la Dunia, Lionel Messi, anashika nafasi ya pili kwenye orodha ya Forbes akiwa ameingiza kiasi cha Dola milioni 130.

10 bora ya Forbes pia ina nyota wa mpira wa kikapu, LeBron James na bondia Canelo Alvarez, huku bingwa mara 20 wa tenisi wa Grand Slam, Roger Federer ndiye mwanamichezo pekee aliyestaafu ambaye yupo kwenye orodha hiyo katika nafasi ya tisa.

Dustin Johnson (wa sita) na Phil Mickelson (wa saba) ndio wachezaji wa gofu wa kwanza kuingia katika 10 bora tangu Tiger Woods mwaka 2020.

Johnson hakuwa katika 50 bora mwaka wa 2022, lakini baada ya kuwa mchezaji wa kwanza wa hadhi ya juu naye amepanda katika orodha ya Forbes.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,109,9
MECHI KALI
BAYER LEVERKUSEN
VERSUS
FC KOLN
1 | 1.61
X | 3.90
2 | 4.70
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# GUARDIOLA: HAALAND ANASTAHILI KULINDWA

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema mshambuliaji, Erling Haaland anastahili kulindwa sana na wachezaji wenzake wa Manchester City baada ya kuvunja rekodi ya kufunga mabao katika msimu mmoja wa Ligi Kuu England.

Haaland alifikisha jumla ya 51 katika mashindano yote juzi usiku, wakati umaliziaji wake mzuri ulipoongeza mabao yake kwenye Ligi Kuu hadi 35 na kuvunja rekodi ya mashindano ya Andy Cole na Alan Shearer.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway alifunga pamoja na Nathan Ake na Phil Foden katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya West Ham.

Baada ya mchezo huo, Guardiola alisema Haaland anastahili ulinzi.

"Ilikuwa (maalum), nadhani anastahili," alisema bosi huyo wa City.

"Timu zote zilistahili kwa sababu bila timu asingeweza kufanya hivyo, lakini ni mshambuliaji maalum.

"Tumefurahishwa sana naye kwa sababu ni mchezaji maalumu. Nadhani kila mtu anafurahi kuwa naye pamoja nasi.

"Kwa kweli rekodi hii itavunjwa mapema au baadaye, labda naye katika siku zijazo au labda nyingine lakini watalazimika kufunga mabao mengi kwa sababu alifunga mengi.



## Madrid yamkomalia Bellingham

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid wana matumaini ya kuwashinda Manchester City katika vita ya kumsajili Jude Bellingham, lakini vyanzo mbalimbali vimeiambia ESPN ni mapema sana kuzungumza juu ya aina yoyote ya makubaliano kufikiwa.

Bellingham (19), ni mmoja wa wachezaji wanaotafutwa sana duniani na ESPN iliripoti kwa mara ya kwanza Madrid kutaka kumnunua kiungo huyo wa Borussia Dortmund Novemba, mwaka jana.

Liverpool walidhaniwa ndio waliopewa nafasi kubwa ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England, lakini kikosi cha Jurgen Klopp kilijiondoa katika kinyang'anyiro hicho mwezi uliopita.

Kufuatia kujiondoa kwa Liverpool, vyanzo viliiambia ESPN mabingwa wa Ligi Kuu England, City walihisi walikuwa kwenye nafasi nzuri zaidi kupata saini ya Bellingham.

75,029/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/05/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Aston Villa | 2.85 | 3.15 | 2.36 |
| 02. 06/05/23 | 18:00 | OGC Nice vs Stade Rennes | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 03. 06/05/23 | 19:00 | AS Roma vs Inter Milano | 2.60 | 3.05 | 2.65 |
| 04. 06/05/23 | 21:45 | US Cremonese vs Spezia Calcio | 2.20 | 3.25 | 3.05 |
| 05. 06/05/23 | 22:00 | RC Lens vs Olympique Marseille | 2.23 | 3.40 | 2.90 |
| 06. 07/05/23 | 00:00 | CA Belgrano vs Atletico Tucuman | 2.20 | 2.95 | 2.90 |
| 07. 07/05/23 | 02:30 | Charlotte FC vs New York City FC | 2.41 | 3.05 | 2.55 |
| 08. 07/05/23 | 02:30 | San Jose Earthquakes vs Los Angeles FC | 2.60 | 3.20 | 2.26 |
| 09. 07/05/23 | 02:30 | Inter Miami CF vs Atlanta United FC | 2.36 | 3.15 | 2.50 |
| 10. 07/05/23 | 13:30 | Umraniyespor vs Sivasspor | 2.75 | 3.15 | 2.16 |
| 11. 07/05/23 | 13:30 | Atalanta BC vs Juventus Turin | 2.31 | 3.25 | 2.85 |
| 12. 07/05/23 | 16:00 | FC Nantes vs Strasbourg Alsace | 2.50 | 3.30 | 2.60 |
| 13. 07/05/23 | 16:00 | AJ Auxerre vs Clermont Foot 63 | 2.25 | 3.20 | 3.00 |
| 14. 07/05/23 | 16:00 | FC Lorient vs Stade Brest 29 | 2.22 | 3.40 | 2.90 |
| 15. 07/05/23 | 17:30 | Maritimo Madeira vs Rio Ave FC | 2.43 | 3.00 | 2.90 |
| 16. 07/05/23 | 18:30 | Newcastle United vs Arsenal FC | 2.40 | 3.40 | 2.65 |
| 17. 07/05/23 | 20:00 | Vitoria SC Guimaraes vs FC Vizela | 2.31 | 3.10 | 3.00 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 05/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:35 | 3443 | Shenzhen vs Shijiazhuang | 2.62 | 3.09 | 2.47 |
| 14:35 | 3670 | Henan Jianye vs Beijing Guoan | 4.31 | 3.49 | 1.69 |
| 14:35 | 4813 | Shanghai Shenhua vs Dalian Aerbing | 1.70 | 3.33 | 4.51 |
| 17:00 | 4604 | Kapaz vs Sabah | 7.06 | 4.36 | 1.37 |
| 18:00 | 3065 | CR Belouizdad vs ES Setif | 1.54 | 3.57 | 5.80 |
| 18:00 | 4090 | Honka vs Lahti | 1.36 | 4.32 | 7.00 |
| 18:00 | 4702 | Isloch vs Slavia Mozyr | 2.01 | 3.43 | 3.22 |
| 18:00 | 5043 | Vyskov vs Pribram | 1.91 | 3.39 | 3.44 |
| 18:00 | 5428 | Haka vs FC KTP | 1.87 | 3.28 | 3.69 |
| 18:00 | 5764 | Seinajoen JK vs Inter Turku | 2.29 | 3.08 | 2.87 |
| 18:15 | 3058 | KuPS Kuopio vs HJK Helsinki | 3.13 | 3.07 | 2.15 |
| 19:00 | 1112 | AL Akhdood vs AL Hazm | 2.14 | 3.14 | 3.09 |
| 19:00 | 3945 | HNK Sibenik vs Vsnk Varazdin | 2.28 | 3.08 | 2.88 |
| 19:10 | 1970 | Amstetten vs First Vienna | 2.22 | 3.42 | 2.80 |
| 19:10 | 3677 | SV Horn vs Rapid Vienna II | 2.20 | 3.38 | 2.86 |
| 19:30 | 2844 | FC Stade LS Ouchy vs Neuchatel Xamax | 1.78 | 3.55 | 3.75 |
| 19:30 | 3148 | Arminia Bielefeld vs Greuther Furth | 2.34 | 3.43 | 2.77 |
| 19:30 | 5488 | Hamburger SV vs Paderborn | 1.94 | 3.79 | 3.33 |
| 20:00 | 2257 | AFC Eskilstuna vs Utsiktens BK | 2.48 | 3.35 | 2.71 |
| 20:00 | 2539 | Torpedo Zhodino vs Slutsk | 1.70 | 3.59 | 4.26 |
| 20:00 | 2698 | Leixoes vs Belenenses | 1.97 | 3.33 | 3.49 |
| 20:00 | 4861 | Duisburg vs Erzgebirge Aue | 2.20 | 3.48 | 2.95 |
| 20:00 | 5881 | JS Kabylie vs USM Alger | 1.77 | 3.21 | 4.46 |
| 20:30 | 1206 | Wolfsberger AC vs SCR Altach | 1.88 | 3.39 | 3.54 |
| 20:30 | 1461 | Yverdon-Sport FC vs Lausanne-Sport | 2.73 | 3.35 | 2.25 |
| 20:30 | 5936 | FC Schaffhausen vs AC Bellinzona | 1.81 | 3.59 | 3.59 |
| 21:00 | 1866 | Dordrecht vs Heracles Almelo | 7.70 | 5.10 | 1.30 |
| 21:00 | 2323 | Telstar vs Willem II Tilburg | 3.80 | 3.43 | 1.85 |
| 21:00 | 4120 | Helmond Sport vs VVV Venlo | 2.75 | 3.27 | 2.35 |
| 21:00 | 5135 | Waalwick vs FC Volendam | 1.83 | 3.75 | 3.60 |
| 21:00 | 5312 | Roda Kerkrade vs FC Eindhoven | 2.39 | 3.34 | 2.66 |
| 21:00 | 5683 | De Graafschap vs Maastricht | 1.53 | 4.27 | 4.80 |
| 21:15 | 4106 | FC Aarau vs FC Wil | 2.11 | 3.39 | 2.93 |
| 21:15 | 5384 | Mouloudia Oujda vs Ittihad Tanger | 2.38 | 2.92 | 2.87 |
| 21:30 | 1526 | Perugia vs Cagliari | 2.98 | 2.98 | 2.39 |
| 21:30 | 3187 | Mainz vs Schalke 04 | 1.60 | 3.90 | 4.80 |
| 21:30 | 3851 | Bayer Leverkusen vs FC Koln | 1.61 | 3.90 | 4.70 |
| 21:45 | 1194 | Cove Rangers vs Morton | 2.92 | 3.44 | 2.17 |
| 21:45 | 1285 | Shelbourne vs UCD Dublin | 1.37 | 4.13 | 7.22 |
| 21:45 | 1803 | Shamrock Rovers vs Bohemians FC | 1.70 | 3.50 | 4.23 |
| 21:45 | 4519 | Inverness vs Ayr United | 2.34 | 3.37 | 2.70 |
| 21:45 | 4571 | Cork City vs St Patricks | 2.87 | 3.23 | 2.21 |
| 21:45 | 4899 | Drogheda Utd vs Derry City | 4.31 | 3.44 | 1.70 |
| 21:45 | 5150 | Queens Park vs Dundee FC | 3.32 | 3.48 | 1.97 |
| 21:45 | 5317 | Arbroath vs Hamilton | 1.97 | 3.33 | 3.49 |
| 21:45 | 5810 | Raith Rovers vs Partick Thisle | 3.84 | 3.64 | 1.79 |
| 22:00 | 5276 | Alaves vs Granada | 2.26 | 3.00 | 3.20 |
| 22:15 | 3213 | Casa Pia Atletico vs Portimonense | 2.10 | 3.21 | 3.36 |
| 23:30 | 2103 | Cusco FC vs Deportivo Municipal | 1.55 | 3.80 | 4.93 |
| 23:30 | 5165 | Union Touarga vs FUS Rabat | 3.89 | 2.97 | 1.94 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# BONDIA AFUNGUKA, AKIMBILIA GHANA KUKWEPA UPENDELEO

Na Saada Akida

BONDIA wa ngumi za kulipwa, Loren Japhet, amesema hayupo tayari kucheza tena pambano dhidi ya Watanzania wenzake kutokana na kutotendewa haki, imeelezwa.

Japhet ametoa kauli hiyo kufuatia madai yake ya kunyimwa ushindi katika pambano dhidi ya Juma Choki lililofanyika mwezi uliopita baada ya mpinzani wake kutangazwa mshindi.

**Bondia huyo alisema kabla ya Kamati ya Ufundi ya Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), kubatilisha ushindi huo kwa kutoa sare baada ya pambano hilo.**

Akizungumza na Nipashe jana, Loren alisema hatapanda ulingoni hapa kwa sababu anaamini amekuwa akionewa na kudai wapinzani wake wamekuwa wakibebwa na majaji.

Bondia huyo ambaye kwa sasa makazi yake yako Ghana alisema anashangazwa kuona hali hiyo imekuwa ikijirudia kila anapokuwa na pambano dhidi ya wapinzani wazawa.

"Sio mara ya kwanza kutokea, kila mmoja ameona lile pambano namna nilivyompiga mpinzani wangu, lakini matokeo yalitangazwa mimi ndiyo nimepoteza, kitu ambacho kwa walioangalia hawawezi kukubali ukweli huo. Nadhani kwa sasa siwezi kukubali kucheza tena na mabondia wa ndani na ndio sababu niliamua kwenda Ghana, nimekuwa nikicheza kwa usawa tofauti na hapa nyumbani," alisema bondia huyo.



Mshambuliaji wa JKT Queens, Stumai Abdallah (kushoto), akipokea tuzo ya Mchezaji Bora wa Ligi ya Wanawake Tanzania (SWPL) wa Aprili kutoka kwa Meneja Masoko Msaidizi wa Rani Sanitary Pad ambao ni wadhamini wenza wa ligi hiyo, Raphia Issa. **PICHA: TFF**

## Robertinho ataka straika

INATOKA UK. 24

kupambana, makosa madogo yalitugharimu lakini sasa tunaangalia mbele kwenye michezo ya ligi iliyobakia na Kombe la FA," alisema Robertinho.

Aliongeza alilazimika kupumzisha baadhi ya nyota wake wa kikosi cha kwanza kutokana na kukabiliwa na mchezo muhimu wa hatua ya nusu fainali ya FA dhidi ya Azam itakayochezwa Jumapili.

Naye Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili baada ya kushindwa kuvuna pointi zote tatu katika mechi hiyo iliyopita, bado malengo yao ni kupambana na kushinda michezo iliyosalia.

Mgunda alisema bila kujali matokeo ya timu nyingine, wao watahakikisha wanapambana kusaka alama tatu ili kumaliza vizuri msimu huu wa ligi.

"Mchezo dhidi ya Namungo umemalizika, tumepata sare, tunarudi kwenye uwanja wa mazoezi kujiandaa na mechi zilizosalia, hatuangalii nani kafanya nini, tunahitaji kushinda mechi zetu zote.

Tulijua isingekuwa mechi rahisi, Namungo ni timu nzuri hasa inapokuwa nyumbani, lakini mpira una matokeo matatu, tunarudi kujipanga kwa mechi zilizopo mbele yetu," Mgunda alisema.

Katika mchezo huo Simba iliwakosa Chama, Enock Inonga, Mzamiru Yassin, Saido Kanoute, Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr'.

## *Yanga yanusa ubingwa Bara*

INATOKA UKURASA 24

CAS, kwa hatua hii hamashauri arudi tu kambini na aje tukae mezani ili kuboresha kile ambacho anakihitaji," alisema Simon.

Naye Fatma Karume alisema waliambiwa walete utetezi kwa maandishi na walifanya hivyo.

"Ninaimani hoja hizo zitafanyiwa kazi, lakini dakika 10 ambazo tumepewa huwezi kuongea hoja ya msingi, huwezi kufafanua hoja hizo, wanasema watatoa uamuzi wao, hivyo tunasubiri, lakini kwa kauli ya kwenda CAS, kwa sababu akishindwa ndio anatakiwa kwenda huko, je, kwa kauli hiyo inamaanisha wao ndio wameshinda," alihoji Fatma Karume.

Michezo

Ijumaa Mei 5, 2023

Nipashe



Haaland anastahili kulindwa UKURASA 22




Winga wa Yanga, Jesus Moloko (kushoto), akijiandaa kumtoka nyota wa Singida Big Stars, Shafiq Batambuze katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Liti ulioko mkoani Singida jana. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Robertinho ataka straika, beki mpya

**Saada Akida na Faustine Feliciane**

WAKATI timu yake ikilazimishwa sare ya bao 1-1 na Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' amesema anahitaji nyota wapya kwa ajili ya kujiandaa na michuano ya Super League inayotarajiwa kufanyika Agosti, mwaka huu.

Robertinho amesema hayo muda mchache baada ya kumalizika kwa mechi hiyo ya ligi alipokutana na mabosi wa Simba katika kikao cha tathmini.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema katika kikao hicho kilichohusisha wajumbe wa bodi waliokuwa mkoani Lindi, Robertinho aliweka wazi anahitaji beki, viungo wawili (mshambuliaji na kiungo mkabaji) pamoja na mshambuliaji ambaye ana ubora zaidi ya Jean Baleke.

Ahmed alisema tayari kocha huyo ameshafanya maboresho ndani ya kikosi cha Simba ambacho kimekuwa na mwendelezo mzuri.

Meneja huyo alisema anaamini wachezaji walioko wana ubora na kinachohitajika ni maboresho ambayo kazi yake imeshaanza kufanyika.

"Kocha amesema anapata changamoto kwa sasa kwa sababu ya mshambuliaji mmoja (Jean Beleke), aliyekuwa naye, lakini pia anataka mbadala wa Chama (Clatous), lengo ni kutengeneza kikosi bora na tishio katika ukanda huu wa Afrika na zaidi kufika hatua ya nusu fainali hadi fainali katika michuano ya kimataifa," Ahmed alisema.

Robertinho aliliambia gazeti hili matokeo hayo yamewapunguzia presha wapinzani wao wakubwa, Yanga ambao wako katika mbio za kuwania ubingwa.

"Wachezaji walijitahidi

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga yanusa ubingwa Bara

## Inahitaji pointi tatu tu kutetea taji huku Fei Toto akigonga mwamba katika...

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

WAKATI mabingwa watetezi, Yanga wakiukaribia ubingwa wa msimu huu baada ya kuichapa Singida Big Stars mabao 2-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani Singida jana, kiungo Feisal Salum 'Fei Toto' ameendelea kugonga mwamba kuhusiana na shauri lake.

**Ushindi huo wa Yanga umeifanya kufikisha pointi 71 na hivyo inahitaji pointi tatu ili ifikishe pointi 74 tu kujihakikishia taji hilo kwa sababu hakuna timu yoyote inayoweza kufikia idadi hiyo.**

Simba iliyoko katika nafasi ya pili na pointi 64 mkononi, endapo itashinda mechi zake tatu zilizobakia itafikisha pointi 73.

Stephano Aziz Ki aliendelea kuwa mwiba kwa magolikipa kutokana na mashuti yake baada ya kufunga bao la kwanza dakika ya 15 kufuatia shuti kali lililomshinda golikipa wa Singida BS, Benedicto Haule kulidaka.

Baada ya kuingia bao hilo, Yanga waliendelea kulisakama lango la wapinzani wao na dakika tano baadaye, Clement Mzize, alitumia vyema krosi ya Jesus Moloko kuandika goli la pili katika mchezo huo.

Mabao hayo yalidumu kipindi chote cha kwanza, kipindi cha pili kilianza kwa kasi huku kila timu ikifanya mabadiliko, Singida BS wakimtoa, Meddie Kagere na kuingia Enock Agyei huku Yanga wakiwatoa kwa nyakati tofauti MoLoko, Mzize na Aziz Ki na nafasi zao kuchukuliwa na Bernard Morison, Salum Abubakary 'Sure Boy' na Fiston Mayele.

Hata hivyo mabadiliko hayo hayakubadili matokeo ya mchezo, zaidi ya wenyeji kujipanga kuzuia mashambulizi yaliyokuwa yakitengenezwa na Yanga.

Pamoja na juhudi za safu ya ushambuliaji ya Singida Big Stars kuweza kupata goli, juhudi hizo zilikuwa zikiishia kwenye safu ya mabeki wa Yanga iliyokuwa chini ya Bakari Mwamnyeto na kipa, Djigui Diarra.

Baada ya mechi hiyo, Yanga ambao ni wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa wataanza kujiandaa na mchezo wake wa kwanza wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Mallumo Gallants ya Afrika Kusini utakaochezwa Mei 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Wakati huo huo, Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), iliyokutana jana ilitumia dakika 27 kusikiliza shauri la Fei Toto na Yanga ambao walipeleka pingamizi la kutaka mchezaji huyo kuvunja mkataba kupitia klabu yao na sio shirikisho.

Fei Toto alifika TFF saa 9: 50 Alasiri na gari aina ya Toyota Alphard namba T564 ECM akiambatana na Wakili, Fatuma Karume 'Shangazi', Jasmin Razack, wakiambatana na mama yake mzazi wa mchezaji huyo.

Yanga ndio walikuwa wa kwanza kufika katika ofisi hizo wakiongozwa na Mtendaji Mkuu wa Yanga, Andre Mtine, Mkurugenzi wa Sheria wa Yanga, Patrick Simon na wanasheria wengine.

Mwanasheria wa Yanga, Simon alisema baada ya kamati kusikiliza hoja zao na kusubiri uamuzi na anaimani suala hili kwa Tanzania limekwisha baada ya kusikilizwa zaidi ya mara tatu.

"Jambo hili limekwisha kwa hapa Tanzania, kama wanahitaji basi linaweza kuamuliwa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002